هذا هو الإسلام - سواحيلي

# Huu ndio Uislamu



جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي

285

هاتف: ٠١٦ ٤٢٣٤٤٦٦ ـ فاكس: ٠١٦ ٤٢٣٤٤٧٧

جمعية الدعوة بالزلفي

# HUU NDIO UISLAM

## هذا هو الإسلام - سواحيلي

KIMETAFSIRIWA NA KUHAKIKIWA NA:

1- ALLY NASSOR ALLY
2- ABDALLAH CHUMBE
3- ABUBAKAR KASSIMU ABUBAKAR


جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات في الزلفي

هاتف: 164234466 966 ـ فاكس: 164234477 966

# هذا هو الإسلام - سواحيلي

**أعده وترجمه للغة السواحيلية**

**جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي**

**الطبعة الأولى: ١٤٤٤/٠٦ هـ**


**ⓗجمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي ، ١٤٤٤هـ**

***فهرسة مكتبة الملك فهد الوطنية أثناء النشر***

جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي
هذا هو الإسلام / لغة السواحلية. / جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي .- الزلفي ، ١٤٤٤هـ
٩٢ ص ؛ ..سم

ردمك: ٦-١٥-٨٣٩٩-٦٠٣-٩٧٨

١- الاسلام ٢- التوحيد أ.العنوان
ديوي ٢١٠ ١٤٤٤/٥٨٢٨

**رقم الإيداع: ١٤٤٤/٥٨٢٨**
**ردمك: ٦-١٥-٨٣٩٩-٦٠٣-٩٧٨**

# Huu ndio Uislamu

# هذا هو الإسلام

## UTANGULIZI

Mtu anapotafakari kuhusu ardhi na kuona ulimwengu huu mkubwa uliyo mzuri, mbingu, sayari na nyota zilizoipamba kwa wingi, na zote zikienda kwa mpango maalumu, anapoona milima, mabonde, mito, mimea mbalimbali, hewa, maji, nchi kavu na bahari, mchana na usiku, bila shaka atatambua kwamba yupo Aliyeviumba vitu vyote hivi na kuviwekea kanuni zake?

Ni nani Anayeteremsha mvua kutoka mawinguni ambayo uhai wa ardhi hupatikana kwayo? Yeye kwa mvua Anaotesha mimea mbalimbali, ambayo baadhi huzaa matunda na mingine maua tu kwa ajili ya kuburudisha nafsi za watu! Watu na wanyama wanapata maji kutokayo kwa ajili ya matumizi yao, na Akaiandaa ardhi kuhifadhi maji hayo. Ni nani Aliyeweka mvutano maalumu kwenye ardhi tena kwa kadiri ya mahitaji ya vitu vilivyomo? Hauzidi na hivyo

kuwa vigumu kusonga juu yake, na wala haupungui na hivyo kufanya vitu visitulizane juu yake?

Ni nani Aliyemuumba mwanadamu kwa ubunifu wa hali ya juu, na kwa sura iliyo nzuri?

Kama mtu atafikiri kwa makini bila shaka ataona maajabu makubwa katika uwezo mkubwa usio na kifani wa Muumbaji wa mbingu na ardhi na vyote vilivyomo Ambaye ni Allah-Mtukufu! Umadhubuti wa Uumbaji Wake ni wa kustaajabisha. Unaweza kufikiri kuhusu viungo vya mwili wako vinavyofanya kazi kwa umakini wa hali ya juu, na wala hamna hata mtu mmoja anayejua hasa namna vinavyofanya kazi isipokua kwa uchache tu, ni vipi basi, wewe utakuwa na uwezo wa kuvidhibiti?

Fikiria fadhila za Allah-Mtukufu zilizo juu yako kwa hewa tu unayopumua kwani kama itasimama kwa muda mfupi tu kwa hakika wewe utapoteza maisha, ni nani Aliyeiweka?

Fikiria kuhusu maji unayokunywa, na asili ya chakula unachokula, na ardhi unayotembea juu yake, na pia mbingu na vilivyo mbinguni, na jua linalotupatia mwanga na kuendeleza uhai wa mimea, na mwezi na nyota na kila unachokiona kwa macho yako, ni nani Aliyeviumba vitu vyote hivyo?

Kwa hakika Aliyeviumba ni Allah-Mtukufu, Yeye Ndiye Muumbaji wa ulimwengu na vyote vilivyomo na ni Yeye tu Peke Yake Ndiye Anaeusimamia na Kuuendesha barabara kama Qur'ani inavyobainisha;

"Allah-Mtukufu Ndiye kamwe hapana Mola Anayepasa kuabudiwa kwa haki ila Yeye tu Peke Yake, Aliye Hai milele, Aliye Mwenye Kusimamia barabara (katika Kuendesha mambo yote). Katu halimshiki yeye lepe wala usingizi. Ni vyake Yeye tu vyote vilivyo mbinguni na vyote vilivyo ardhini. Na ni nani huyo (yaani hapana yeyote) ambaye ataombea (mwingine) mbele Yake Yeye ila kwa Idhini Yake. Yeye Anayajuwa vyema yote yaliyo mbele yao (hao viumbe) na yote yaliyo nyuma yao (yaani katika mambo ya Duniani na ya huko Akhera). Na katu wao (hao viumbe) hawajui chochote katika Kujua Kwake ila kile ambacho Yeye Anataka. Imeenea *Qursiiy* Yake zile mbingu na ile ardhi, hali ya kuwa katu hakumchoshi Yeye kuvilinda hivyo viwili. Na daima Yeye Ndiye Aliye Mtukufu zaidi, Aliye Mkuu Asiyemithilika." [Al-Baqarah, Q2:255].

Yeye Ndiye Mola wako Mlezi Aliyekuumba, Anayekupa riziki, na Ndiye Anayekupa maisha, uhai na Ndiye Anayekufisha unapofika muda wako Alioukadiria na Yeye Ndiye Aliekufanya uwepo baada ya kuwa Si lolote.

Baada ya kuyajua haya yote, hivi kuna yeyote mwenye akili timamu anayeweza kudhani kwamba huu ulimwengu umeumbwa kwa ajili ya mchezo tu, na kwamba watu wanazaliwa na kuishi kwa muda kisha wanakufa na ndio unakua mwisho wao hakuna jingine tena!

Basi ni nini uhakika wa jambo hili?

## KWA NINI TUMEUMBWA?

Allah-Mtukufu Ndiye Aliyetuumba sisi kwa Kutaka Kwake, halafu Akawatuma kwetu sisi wale Mitume na Manabii (kama wajumbe Wake) na Akateremsha pamoja na baadhi yao Vitabu, ili wapate kutufundisha ni vipi sisi tutamuabudu Yeye? Kwa hivyo yeyote atakaemuabudu Allah-Mtukufu kwa kumtakasia ibada na akatii amri Zake na akiepuka yote yale Aliyokataza, yeye atapata Radhi Zake. Na atakayeacha kumuabudu na akakataa kutii Amri Zake yeye atastahili Ghadhabu na Adhabu Yake.

Allah-Mtukufu Ameifanya hii dunia kuwa nyumba ya matendo na mitihani.

Kisha siku ya Kiyama Allah-Mtukufu Atawafufua watu wote kwa ajili ya kuhesabiwa na kulipwa kwa mujibu wa matendo yao. Na Allah-Mtukufu Ameandaa pepo

yenye neema nyingi ambazo katu hazijapata kuonwa na jicho la mtu yeyote, wala kusikiwa na sikio la mtu yeyote, wala kuwazwa na moyo wa mtu yeyote, kwa ajili ya waja wake wale waliyo wema, wale waliyomuamini na kutii Amri Zake.

Na Ameandaa pia Moto ambao mna ndani yake kila aina ya adhabu ambazo hazijawahi kuwazwa katika akili ya mtu yeyote, huo Moto Allah-Mtukufu Ameuandaa kwa kila aliempinga, na akamuabudu shetani na akafuata dini mbali na Uislamu.

## UISLAM NI NINI?

Uislam ndio Dini inayoridhiwa na Allah-Mtukufu, ni Dini inayomtaka mtu amuabudu Yeye tu Peke Yake na kumtii Mtume Wake Muhammad-Rehema na Amani ya Allah-Mtukufu- iwe juu yake.

Na Allah-Mtukufu Hatamkubalia mtu yeyote atakayefuata Dini kinyume na Uislamu, na Uislam Si Dini maalum kwa ajili ya baadhi ya watu, bali ni Dini ya Allah-Mtukufu kwa ajili ya watu wote.

Allah-Mtukufu Amewaamrisha waja Wake Amri nyingi, na Amewakataza mambo yote ya haramu, yeyote atakaemtii atafaulu, na yeyote atakayemuasi ataangamia na kupata hasara.

Uislam Si dini mpya, bali ni Dini ambayo Allah-Mtukufu Ameichagua kwa ajili ya waja wake tokea Kuumbwa kwa dunia, na ndio Dini iliyolinganiwa na Mitume Wake wote-Rehema na amani ziwe juu yao.

## KUUMBWA KWA NABII ADAMU

Kabla ya kuumbwa kwa Nabii Adamu-Alayhi salaam Allah-Mtukufu Aliwaarifu Malaika kuhusu kusudio Lake kama Qur'ani inavyobainisha;

"Na (ewe Mtume Muhammad-Swallallaahu alayhi wasallama kumbuka) wakati Mola wako wewe Alipowaambia Malaika; "Kwa hakika Mimi Nitaweka katika ardhi Khalifa (yaani kiongozi)" wao wakasema; "Hivi! Wewe Utaweka humo wale ambao wataeneza ufisadi humo na kumwaga damu, wakati sisi tunakusabihi na kukusifu na kukutakasa Wewe?" Yeye Akasema; "Kwa hakika Mimi Ninayajuwa yale ambayo katu nyinyi hamjuwi." [Al-Baqarah, Q2:30].

Ndiyo baadaye Allah-Mtukufu Akamuumba baba yetu Adamu-Amani iwe juu yake pale Alipomuumba kwa udongo, kisha Akaupulizia roho, na Kumfundisha yeye majina ya vitu vyote, na Akawaamrisha Malaika wamsujudie, ikiwa ni katika kumkirimu na kumtukuza kwa elimu yake. Wakamsujudia wote isipokuwa Ibilisi alifanya kiburi na kukataa, kwa husda tu dhidi ya

Nabii Adamu. Mwenyezi Mungu Akamfukuza kutoka mbinguni na kumtoa hali ya kuwa dhalili na myonge. Na Akamlaani na Kumfanya miongoni mwa viumbe wenye maisha mabaya duniani na Akhera na Akaahidiwa kuingizwa katika Moto wa Jahanamu yeye pamoja na wote watakaomfuata.

Basi, Ibilisi akaomba kwa Mola wake mlezi Amuakhirishe, yaani asife mpaka Siku ya Kiyama, na Yeye Akamkubalia ombi lake! Kwa chuki dhidi ya Nabii Adamu na uzao wake akaapa kuwa atahakikisha anawapotosha wana wa Adamu wote, na kuwaondoa kwenye njia iliyo nyooka na sahihi iliyo ya haki (yaani Uislamu).

Kisha baada ya hapo Allah-Mtukufu Akamuumba mkewe Hawaa ili apate utulivu na kiliwazo kwake, na Akawaamrisha wakae Peponi, ambamo mna kila aina ya neema, ambazo hazijapata kuonwa na mtu yeyote hapa duniani. Na Allah-Mtukufu Akawaeleza wazi juu ya uadui wa Ibilisi kwao, na Akawakataza wao kula kutoka katika mti fulani humo peponi, kama mtihani kwao, lakini Shetani akawashawishi na kuwapambia kula kutoka katika mti ule, na akaapa kwao kuwa yeye ni mshauri mzuri na akawahadaa kwa kuwaambia; ‘Kama nyinyi mtakula kutoka katika mti huu mtakuwa watu mtakaoishi milele na kamwe hamtakufa.’

Basi hakuacha kuwashawishi mpaka alipofaulu kuwatelezesha na hivyo kuwapotosha, wakala tunda la mti ule na kumuasi Allah-Mtukufu Mlezi wao. Basi, walipoligundua hilo walijuta sana kwa hicho kitendo chao, na wakatubia kwa Mola wao mlezi, baada ya Yeye Kuwafundisha maneno ya kuombea toba Kwake, na Mola wao akawakubalia toba yao, lakini Akawateremsha kutoka Peponi na kuwaleta wao duniani. Adamu akaishi na mkewe duniani, na wakajaaliwa kuzaa watoto wengi na watu wanaendelea hivyo mpaka leo hii.

Na Ibilisi na kizazi chake nao wanaendelea na vita yao dhidi ya wanadamu, ili wawazuie kufuata uongofu na kuwanyima kheri, na kuwapambia mambo yaliyokatazwa ili apate kuwaweka mbali na yale ambayo yanamridhisha Allah-Mtukufu na shauku yake kubwa ni kuingia nao Motoni Siku ile ya Kiyama.

Lakini kama Allah-Mtukufu Alivyowaahidi Hakuwaacha viumbe wake bila ya msaada, bali Aliwatumia Mitume kwa ajili ya kuwakumbusha na kuwabainishia wao njia ya haki, na kuwaelekeza wao kwenye vile vitendo vyenye manufaa kwao.

Hata baada ya Nabii Adam-Alayhi salaam kufariki kizazi chake kiliishi kwa zaidi ya karne kumi, wakiendelea kumtii Allah-Mtukufu na kumpwekesha

kama walivyousiwa na baba yao! Baada ya muda mrefu kupita ukatokea ushirikina miongoni mwao na watu wakaanza kuabudu asiyekuwa Allah-Mtukufu pamoja Naye, watu wakawa wanaabudu masanamu! Basi, Allah-Mtukufu Akatuma Mtume wake Nabii Nuhu–Amani iwe juu yake baada ya Nabii Adamu, ili kuwalingania watu wapate kumuabudu Allah-Mtukufu tu Peke Yake Asiye na mshirika kama ilivyo ada na waache kuabudu Masanamu.

Kisha ikafululiza Mitume baada ya Nabii Nuhu, wakiwalingania watu kwenye kuufuata Uislamu, ambao ni imani ya kumuabudu Allah-Mtukufu tu Peke Yake na kuacha kuabudu kitu kingine chochote kinyume Naye.

Kisha akafuata Nabii Ibrahim - Amani iwe juu yake - na yeye pia akawalingania watu wake kuacha kuabudu masanamu, na akawa Anawahimiza kumuabudu Allah-Mtukufu tu Peke Yake.

Na Utume baada ya Nabii Ibrahim ukaenda kwa watoto wake Nabii Ismaili, Is-haka, na ukaendelea hivyo kwa muda mrefu katika kizazi chao.

Na Mitume wakubwa kutoka kizazi cha Nabii Is-haka ni Nabii Ya'aqub, Yusuf, Musa, Daudi, Suleimani na Nabii Isa-Amani iwe juu yao. Na baada ya Nabii Isa

hapakuwa na Mtume mwingine tena kutoka katika kizazi cha Nabii Is-haka.

Baada ya hapo Utume ukahamishiwa kwa kizazi cha Nabii Ismail, pale Allah-Mtukufu alipomdhihirisha Mtume Muhammad-Amani iwe juu yake kama Nabii na Mtume wa mwisho kutoka Kwake kwa wanadamu wote, na ujumbe wake ukafanywa kuwa wa mwisho, na Kitabu chake, yaani Qur'ani ndio Kitabu cha mwisho kutoka kwa Allah-Mtukufu.

Na ndio sababu ujumbe wake umeenea katika kona zote za dunia, umekamilika! Kutoka mwanzo ulikusudiwa kuwa wa watu wote pamoja na majini, kwa waarabu na wasio waarabu, ni wenye kufanya kazi zama zote, mahali popote na katika jamii yoyote, na kwa hali zote, hakuna heri isipokuwa umeielekeza na wala hakuna shari isipokuwa ujumbe umeitahadharisha.

Na Allah-Mtukufu Hatakubali kutoka kwa mtu yeyote Dini yeyote kinyume na Dini ya Uislamu, ile aliyokuja nayo Mtume Muhammad - Rehema na amani ya Allah-Mtukufu iwe juu yake!

## Mtume Muhammad - Rehema na Amani ya Allah-Mtukufu iwe juu yake:

Kwa hakika Allah-Mtukufu Amemtuma Mtume Muhammad-Rehema na amani ya Allah iwe juu yake na Yeye Akamfanya yeye kuwa Mtume wa mwisho na Akaufanya ujumbe wake pia kuwa ujumbe wa mwisho.

Allah-Mtukufu Amemtuma Mtume Muhammad-Rehema na amani ya Allah iwe juu yake ili apate kuwaongoza watu kwenye kumuabudu Allah-Mtukufu tu Peke Yake na kuacha kuabudu mashetani mbali na Allah-Mtukufu kama vile masanamu, mizimu na kadhalika.

Na Mtume Muhammad - Rehema na amani ya Allah- iwe juu yake alikuwa mtu mwenye kusifika kwa tabia njema katika jamii yake, kama vile ukweli, uaminifu, na adabu za hali ya juu, mpaka jamaa zake wakafikia hatua ya kumuita mtu aliye muaminifu. Mtume Muhammad - Rehema na amani ya Allah iwe juu yake alipewa Utume akiwa na umri wa miaka arobaini katika mji mtukufu wa Makka.

Yeye alikua hajapata kusomi Kitabu chochote cha Dini kabla ya kuteremshiwa Qur'ani wala hakuwa anaandika (*Ummiyyi*). Kupitia kwa Malaika Jibrilu -

Alayhi salaam, Allah-Mtukufu Akamfundisha yeye kusoma Qur'ani tukufu ambayo viumbe wote mpaka leo hii wameshindwa kuleta mfano wake.

## Nasaba na Maisha Yake kwa Ufupi - Rehema na Amani ya Allah - Mtukufu iwe juu yake.

Yeye ni Muhammad, mtoto wa Abdallah, mtoto wa Abdul-Mutwalib, mtoto wa Hashim, anaetokana na kizazi cha Nabii Ismaili, mtoto wa Nabii Ibrahim - Amani iwe juu yao.

Mama yake ni Amina binti Wahabi, mtoto wa Abdul Manafi, mtoto wa Zuhrah, na Zuhrah ni ndugu wa babu yake Mtume - Rehema na amani ya Allah - iwe juu yake. Abdullah alimuoa bibi Amina mama yake Mtume - Rehema na amani ya Allah - iwe juu yake, na akaishi pamoja nae kwa muda wa siku tatu, haukupita muda mrefu akapata uja uzito wa Mtume - Rehema na amani ya Allah - iwe juu yake na inasemwa katu yeye hakupata kuona mambo yaliyozoeleka kuonwa na wanawake wajawazito.

Mtume Muhammad - Rehema na amani ya Allah iwe juu yake alizaliwa mwenye sura nzuri na umbo lisilo na kasoro yoyote, na kuzaliwa kwake kulikuwa katika mwaka mia tano na sabini na moja (571) Miladiya.

Baba yake Mtume alifariki kabla ya kuzaliwa kwake, na aliesimamia malezi ya Mtume-Rehema na amani ya Allah iwe juu yake ni babu yake Abdul Mutwalib na alinyonyeshwa na mama yake kwa muda wa siku tatu, kisha akaenda kunyonyeshwa na bibi Halima Saadiya, aliyekua anaishi katika kijiji kimoja pembezoni mwa mji wa Makka.

Na ilikua desturi ya Waarabu kupeleka watoto wao vijijini kwa ajili ya kunyonyeshwa na akina mama waliokuwa na watoto wachanga kwa ujira. Wao walikuwa wanaamini kuwa huko vijijini kunapatikana kwa wingi hali za kumuwezesha mtoto kukua kiakili na kimwili katika afya njema.

Kwa hakika bibi Halima binti Saadiya alianza kuona miujiza mara tu alipomchukua Mtume-Rehema na amani ya Allah iwe juu yake na kuanza kumnyonyesha. Miongoni mwa miujiza ni kwamba bibi Halima binti Saadiya alifika mji wa Makka pamoja na mumewe akiwa na Ngamia aliekonda asiyeweza kutembea vizuri. Wakati akirudi hali ya kuwa amemuweka Mtume - Rehema na amani ya Allah iwe juu yake mapajani mwake wakiwa juu ya ngamia, ngamia huyo aliongeza kasi na kuwaacha nyuma wanyama wote waliokuwa wamefuatana pamoja naye, jambo ambalo liliwashangaza watu wote waliokuwa katika msafara huo.

Kama bibi Halima Alivyopata kusimulia kwamba chuchu zake hazikuwa zinatoa maziwa ya kutosha isipokua machache, na kwa hakika mtoto wake aliyekua akimnyonyesha kabla ya kumchukua Mtume -Rehema na amani ya Allah iwe juu yake alikua akilia kwa muda mrefu kwa sababu ya njaa, lakini alipoanza tu kumnyonyesha Mtume - Rehema na amani ya Allah iwe juu yake chuchu zake zilianza kutoka maziwa mengi kiasi cha kuwatosha watoto wote na mengine kubaki!

Na amesimulia pia kwamba wakati huo kulikua na ukame katika miji ya Saadi, lakini alipofika Mtume - Rehema na amani ya Allah iwe juu yake, hali ilibadilika ghafla kutoka kwenye ukame na kuwa ardhi yenye rutuba ya kutosha, nzuri, na jambo likatoka kwenye ugumu na kuwa jepesi.

Mtume-Rehema na amani ya Allah iwe juu yake aliishi akilelewa na kunyonyeshwa na bibi Halima kwa muda wa miaka miwili, na alikua na hima katika kumlea kwake, na katika kipindi hicho yeye aliona vitu vingi na hali zisizo za kawaida kwa mtoto huyo.

Baada ya miaka miwili kupita bibi Halima alimpeleka Mtume kwa mama yake na babu yake katika mji wa Makka, lakini bibi Halima ambaye tayari alikuwa ameona baraka nyingi za Mtume Muhammad-

Rehema na amani ya Allah iwe juu yake, zilikuwa zimemuathiri kiasi cha kutosha na kwa hivyo akamshawishi mama wa Mtume bibi Amina akubali abaki nae kwa mara ya pili na bibi Amina akakubali ombi lake.

Na hivyo bibi Halima akarejea nyumbani kwa Bani Saadi akiwa pamoja na yule mtoto aliyekuwa yatima (yaani Mtume Muhammad - Swallallaahu alayhi wasallama), akiwa mwenye kutulia na furaha tele.

Baada ya miaka miwili kupita bibi Halima alimrejesha kwa mama yake kwa mara ya pili, na umri wa Mtume Muhammad - Rehema na amani ya Allah iwe juu yake wakati huo ulikuwa miaka minne, akalelewa na mama yake mpaka mama yake alipofariki yeye akiwa na miaka sita, baada ya hapo akaenda kulelewa na babu yake Abdul-Mutwalib kwa muda wa miaka miwili kisha na yeye akafariki, hapo Mtume akaenda kulelewa na ami yake Abu Twalib na akamlea vizuri kama alivyokua akiwalea watoto wake, juu ya kutokuwa na hali nzuri ya kimaisha.

Hata hivyo Mtume Muhammad - Rehema na amani ya Allah iwe juu yake hakuwa amezoea maisha ya starehe, kwani kutoka utoto wake maisha yake yalikuwa ya kawaida, yeye alikuwa amezowea kuchunga mbuzi na kondoo pamoja na ndugu zake

wa kunyonya katika kijiji cha Bani Saadi, hivyo basi, yeye akawa mchunga mbuzi wa watu katika mji wa Makka. Mtume Muhammad - Rehema na amani ya Allah iwe juu yake akawa anampa baba yake mdogo kile alichokua anapata kama ujira wa kazi hiyo!.

Wakati mmoja katika maisha yake Mtume Muhammad-Rehema na amani ya Allah iwe juu yake alisafiri na baba yake mdogo kuelekea Shamu kibiashara, wakati huo akiwa na mika kumi na miwili, kisha akasafiri kwa mara ya pili akiwa kama mfanyabiashara wa mama Khadija binti Khuwaylid, aliyekuwa mwanamke tajiri mkubwa miongoni mwa wanawake wa Makka, Mtume Muhammad-Rehema na amani ya Allah iwe juu yake, yeye aliporudi kutoka safari hiyo alipewa ujira mkubwa tofauti na watu wengine kwa sababu alirejea na faida kubwa.

Baada ya hapo akawa anashiriki katika msafara wa kibiashara kwenda Shamu, na mama Khadija alichangia mali nyingi katika biashara hiyo. Mama Khadija alikuwa mwanamke mjane aliyefiwa na mume na alikuwa miongoni mwa matajiri wakubwa katika mji wa Makka na msimamizi wa mali zake katika msafara huo alikuwa kijana wake aliyekuwa akiitwa Maisara. Kwa sababu ya baraka za Mtume na uaminifu wake biashara ya mama Khadija ilipata faida kubwa ambayo haikuwahi kupatikana huko

nyuma! Mama Khadija akamuuliza Maisara kijana wake sababu ya kupatikana faida kubwa hivyo na yeye akamwabia kwamba Muhammad Mtoto wa Abdillah ndie aliyesimamia mauzo, watu wakajitokeza kwa wingi na hivyo kupata faida kubwa bila ya ulaghai wa aina yoyote katika biashara!

Mama Khadija akamsikiliza kijana Maisara kwa makini na kwa kuwa tayari alikuwa anajuwa baadhi ya mambo kuhusu Mtume Muhammad-Swallallaahu alayhi wasallama, basi akazidi kupendezwa nae na hatimaye akapenda yeye awe mumewe! Siku moja akamtuma mmoja wa watu wake wa karibu ili kwenda kwa Mtume Muhammad-Rehema na amani ya Allah iwe juu yake na kumfikishia ujumbe huo ili apate kujua mtazamo wake juu ya jambo hilo. Wakati huo Mtume alikuwa na umri wa miaka ishirini na mitano, akafikiwa na huyu mjumbe ambaye alimueleza jambo la mama Khadija kuolewa nae, Mtume - Rehema na amani ya Allah iwe juu yake akakubali na kuridhia jambo hilo na ndoa ikafungwa. Kila mmoja alimfurahia na kumridhia mwenzake, kuanzia wakati huo Mtume Muhammad-Swallallaahu alayhi wasallama akawa anaongoza biashara za mama Khadija, na akathibitisha uwezo na umahiri wake mkubwa katika kufanya biashara.

Baada ya miaka kadhaa Allah-Mtukufu Akawabariki na wakapata watoto kadhaa wa kike ambao ni Zainabu, Ruqaiya, Ummu Kulthum na Fatma, na watoto wa kiume wawili Kasimu na Abdallah na hawa wakiume walifariki wakiwa bado wadogo.

Na alipokaribia kufikisha miaka arobaini katika umri wake akaanza kupenda kujitenga na kwenda kwenye pango la Jabal Hiraa, mlima unaopatikana mashariki mwa mji wa Makka, akawa anakaa humo kwa siku kadhaa mfululizo akimuabudu Allah-Mtukufu, Mola wake.

Basi, ulipofika usiku wa tarehe ishirini na moja katika mwezi wa Ramadhani yeye akiwa ndani ya pango hilo, wakati huo akiwa na miaka arobaini, alijiwa na Malaika Jibrilu - Amani iwe juu yake - hapo Jabal Hiraa na yeye akamwambia Mtume Muhammad - Rehema na amani ya Allah iwe juu yake; Soma! Na Mtume akajibu; 'Mimi sijui kusoma.' Malaika Jibrilu akarudia tena kumtaka asome kwa mara ya pili na ya tatu, mara ya tatu akamwambia; "Soma kwa Jina la Mola wako Yule Aliyeumba (kila kitu). Yeye Amemuumba mtu kutokana na pande la damu. Soma na Mola wako ni karimu mno. Yule Aliyefundisha (kuandika) kwa kalamu. Yeye Amemfundisha mtu yale ambayo katu yeye hakuwa anayajuwa." [Al-Alaq, Q96:1-5].

Kisha Malaika Jibrilu akaondoka na kumwacha Mtume, lakini Mtume - Rehema na amani ya Allah - iwe juu yake hakuweza kuvumilia kubaki pale pangoni, akarudi nyumbani kwake na kuingia kwa mkewe mama Khadija hali ya kuwa anatetema kwa hofu, na huku akisema; "Nifunikeni nifunikeni," wakamfunika mpaka hofu ilipomtoka na hapo akamsimulia mama Khadija kile kilichomtokea na akasema; "Kwa hakika nilipata hofu kubwa mno katika nafsi yangu" na mama Khadija akasema; "Naapa kwa Jina la Allah-Mtukufu kamwe Yeye Hatokufedhehesha wewe! Wewe unasaidia wale wasiojiweza na wale masikini, unakirimu wageni na unasaidia katika kuyapatia ufumbuzi matatizo ya dunia."

Basi, baada ya kipindi kifupi Mtume - Rehema na amani ya Allah iwe juu yake alirejea tena Jabal Hiraa kuendelea na ibada zake kwa Allah-Mtukufu. Alipomaliza ibada yake alitoka pangoni ili kurejea Makka, alipokuwa katikati ya bonde, Malaika Jibrilu akamtokea tena akiwa amekaa juu ya kiti kati ya mbingu na ardhi, na akamteremshia yeye Wahyi; "Ewe uliyejigubika (maguo). Simama na uonye (watu kuhusu adhabu kama wao hawakuamini). Na Mola wako Umtukuze. Na nguo zako uzitwaharishe. Na

endelea kujitenga na (mambo) machafu (ya kuabudu masanamu na kadhalika). [Al-Mudathir, Q74:1-5].

Baada ya hapo ndio Wahyi ukawa unateremshwa kwa Mtume Muhammad - Swallallaahu alayhi wasallama mpaka alipotawafu.

Na Allah-Mtukufu Akawa Amemuagiza Mtume Muhammad-Rehema na amani ya Allah iwe juu yake kuwalingania watu katika kumuabudu Allah-Mtukufu tu Peke Yake, yaani jambo la Tauhidi na kuingia katika Dini ya Uislamu, Dini pekee ambayo Allah-Mtukufu Ameiridhia kwa watu na Mtume-Rehema na amani ya Allah iwe juu yake akawa anawalingania watu kwa hekima na kwa mawaidha yaliyo mazuri kama alivyoamrishwa ndani ya Qur'ani;

'Lingania kwenye Dini ya Mola wako kwa hekima na mawaidha yaliyo mazuri na jadiliana nao kwa njia iliyo bora. Kwa hakika Mola wako Ndiye Anayemjuwa vyema yule aliyepotoka mbali na njia Yake na Ndiye Anayemjuwa vyema yule aliyeongoka (na hivyo Yeye Atawalipa wao kila mmoja kwa mujibu wa matendo yake). " [An-Nahl, Q16:125].
Na wa mwanzo kabisa kumuamini ni mke wake mama Khadija, na katika watu wazima ni rafiki yake Sayyidina Abubakar Swidiiq - *Radhiyallaahu anhu*, na katika watoto ni mtoto wa ami yake Sayyidina Ally

bin Abi Twalib - *Radhiyallaahu anhu*, kisha watu wengine wakafululiza kuingia katika Dini ya Allah - Mtukufu. Walipoona hivyo, washirikina wakazidisha uadui na maudhi kwa Mtume-Rehema na amani ya Allah iwe juu yake, na yeye hakusita kwa sababu hiyo isipokuwa aliongeza juhudi na kuendelea kuwalingania watu katika mji wa Makka kwa kipindi cha miaka kumi na mitatu, na yakazidi maudhi ya washirikina kwake yeye na Maswahaba zake, basi, wakati huo ndio Allah-Mtukufu Akamuamrisha kuhama yeye pamoja na Maswahaba zake na kwenda kuishi katika mji wa Madina, na huko aliendelea kulingania watu kuingia katika Uislam! Baada ya miaka mingi alirejea tena katika mji wa Makka kwa kuuteka na wakazi wake wengi wakaingia katika Uislamu.

Alipofikisha miaka 63, Mtume-Rehema na amani ya Allah iwe juu yake alitawafu, alikuwa ameishi miaka arobaini kabla ya Utume na miaka ishirini na mitatu akiwa Mtume.

Na kwake yeye ndio Allah-Mtukufu Amekamilisha Dini na jambo la Utume kutoka mbinguni na Akalazimisha watu wote kumtii na Ameahidi pia kwamba yeyote atakaemtii atapata maisha mazuri hapa duniani na ataingia Peponi kesho Akhera, na yeyote atakayempinga atakuwa na maisha mabaya hapa

duniani (kwa Allah-Mtukufu Kumuondolea furaha na amani ya kweli moyoni mwake), na kesho Akhera ataingia motoni.

Baada ya Mtume wa Allah-Mtukufu-Rehema na amani ya Allah iwe juu yake kutawafu, Maswahaba zake waliendeleza mwenendo wake, na kazi yake ya kulingania na kueneza Dini ya Kiislamu duniani.

## Tabia za Mtume Muhammad - Rehema na amani za Allah-Mtukufu iwe juu yake.

Mtume Muhammad - Rehema na amani ya Allah- iwe juu yake alisifika kwa tabia njema kabla ya Utume na hata baada ya Utume, kimsingi hakupata kusifika kwa tabia mbaya hata moja katika uhai wake. Na ndio ndani ya Qur'ani Allah-Mtukufu Amesema katika kumsifu yeye; "Na kwa hakika wewe U juu ya tabia njema kabisa. [Al Qalam, Q68:4]

Maana hata watu waliokuwa wakipinga hawakupata kumtuhumu kwa tabia mbaya! Mtume-Rehema na amani ya Allah iwe juu yake ni mfano mzuri wa kuigwa na kufuata pia yale anayosema kuhusu hukumu na nasaha mbali mbali.

Kwa hakika Mtume - Rehema na amani ya Allah - iwe juu yake alikuwa kigezo kizuri kwa Maswahaba zake

na alikuwa akiwahimiza kufuata mwendo wake na hivyo kupandikiza tabia zake kwa Maswahaba zake kwa kuonyesha mfano usioyumba.

Kama alivyopata kusimulia Swahaba Sayyidina Anas bin Malik - Allah-Mtukufu Amuwie radhi kwa kusema; "Mimi nimemtumikia Mtume-Rehema na amani ya Allah iwe juu yake kwa miaka kumi, kamwe yeye hakuwahi kuniambia; 'Kwa nini wewe haukufanya hili au kwa nini wewe umefamya hili?'

Na Sayyidina Anas - Radhi ya Allah - Mtukufu iwe juu yake anaendelea kusimulia; "Siku moja mimi nilkuwa nimefuatana na Mtume-Rehema za Allah iwe juu yake akiwa amevaa Joho zito, ghafla akatokea bedui mmoja (yaani Mwarabu wa mashambani) akamvuta kwa nguvu, mpaka nikaona athari ya kuvutwa huko juu ya ngozi ya shingo ya Mtume - Rehema na amani ya Allah - iwe juu yake, kisha yule bedui akasema; 'Ewe Muhammad amrisha mimi nipewe katika mali za Allah-Mtukufu ulizonazo!' Nikashangazwa na nikageuka kumtazama Mtume wa Allah-Mtukufu, nikamuona akicheka na kisha akaamrisha yule bedui apewe chochote".

Wakati mmoja mama Aisha - Radhi ya Allah -Mtukufu iwe juu yake ambaye ni mke kipenzi wa Mtume Muhammad - Rehema na amani ya Allah -Mtukufu iwe juu yake alipata kuulizwa kuhusu mambo

ambayo Mtume - Rehema na amani ya Allah-iwe juu yake alikuwa akifanya akiwa nyumbani kwake? Yeye akasema; *"Alikuwa akifanya kazi za nyumbani kwa kuwasaidia wake zake, ukifika wakati wa swala anatawadha na kwenda kuswali."*

Na Swahaba Abdallah Ibn Harith anasimulia; *"Mimi sijapata kumuona mtu yeyote mwenye tabasamu nzuri kuliko Mtume wa Allah-Mtukufu-Rehema na amani ya Allah iwe juu yake".*

Na Sayyidina Jabir - Allah-Mtukufu Amuwie radhi amesema; "*Mtume hajapata kuombwa kitu chochote cha halali na yeye akakataa kutoa.'*

Na sifa nyingine inayotambulika vyema miongoni mwa tabia njema alizokuwa nazo Mtume - Rehema na amani ya Allah iwe juu yake ni ukarimu, hakuwa bakhili hata kidogo na alikuwa imara na shujaa mkubwa katika kutetea haki, alikuwa muadilifu katika hukumu, hakupata kumdhulumu mtu yeyote katika maisha yake, alikuwa mkweli na muaminifu wakati wote katika maisha yake yote.

Alikuwa akipenda kufanya utani na Maswahaba zake. Na alikuwa akichanganyika nao katika mambo yao ya kijamii. Na alikuwa anapenda kucheza na watoto wao, akiwakalisha katika mapaja yake na kusema nao. Alikua mwepesi wa kuitikia mwaliko. Alikuwa

akitembelea wagonjwa na akikubali udhuru unapotelewa mbele yake. Na alikua akiwaita Maswahaba zake kwa majina wanayopenda na hakuwa anakata mazungumzo ya yeyote miongoni mwao.

Abu Qatada anasimulia; 'Wakati mmoja ulikuja ugeni kutoka kwa mfalme Najashi wa Uhabeshi, Mtume - Rehema na amani ya Allah iwe juu yake alisimama mwenyewe na kuwahudumia, Maswahaba zake wakamwambia; 'Sisi Tunakutosha.' Lakini yeye akasema; *"Kwa hakika wao walikuwa wakarimu kwa wenzetu walipokwenda kwao na mimi napenda kuwalipa wao kwa wema wao."*

Mara nyingi Mtume - Rehema na amani ya Allah - iwe juu yake, alikuwa akisema; *"Kwa hakika mimi ni mja, ninakula kama wanavyokula waja wengine na ninakaa kama wanavyokaa waja wengine."*

Mtume - Rehema na amani ya Allah iwe juu yake wakati mwingine alikuwa akipanda punda na kuwatembelea masikini na watu wanaokaa na mafakiri.

Mwana falsafa maarufu wa Kiingereza Thomas Carlyle ambae alipata kushinda zawadi ya Nobel, katika kitabu chake [Mashujaa] amepata kusema; "Kwa hakika ni aibu kubwa kwa mtu yeyote katika

zama hizi kukubali kuwa Dini ya Uislamu ni ya uongo na Muhammad ni mzushi mwenye kudanganya."

Na Mwingereza mwingine ambaye ni mwandishi maarufu Bernad Show katika kitabu chake (Muhammad) ambacho kilichomwa moto na Utawala wa Uingereza aliandika; "Kwa hakika ulimwengu unahitajia mno mtu mwenye fikra na busara kama Muhammad na Dini yake aliyokuja nayo, huyu Mtume ambae ameifanya Dini yake kuwa yenye kuheshimika na kutukuzwa wakati wote, kwa hakika Dini aliyokuja nayo ndio yenye nguvu zaidi kuliko Dini zote katika kuondoa matatizo ya kijamii, kiuchumi na hata kisiasa. Ni Dini itakayobaki milele, na mimi nimewaona wengi miongoni mwa watu wangu wakiingia katika Dini hii waziwazi na bila shaka Dini hii itapata nafasi kubwa sana katika bara la Ulaya miaka ijaayo."

Na akaendelea kusimulia; "Kwa hakika viongozi wa dini ya Kikristo katika karne za kati, kwa sababu ya ujinga na ubaguzi, waliipa Dini ya Muhammad sifa mbaya, waliitazama kama Dini adui kwa Ukristo, lakini mimi nimechunguza kuhusu Muhammad na kugundua kwamba alikuwa mtu wa ajabu na nikatambua kuwa yeye Si adui wa Ukristo, bali anapasa kuchukuliwa kama mwokozi wa watu, na kwa rai yangu hakika kama mtu huyu angetawala

ulimwengu leo, bila shaka angewezesha kuondoa matatizo yote, na kueneza amani na usalama unaohitajiwa na watu wote siku hizi."

## Baadhi ya Miujiza ya Mtume - Rehema na Amani ya Allah - Iwe Juu Yake.

Mtume Muhammad-Swallallaahu alayhi wasallama ana miujiza mingi ya kutosha na muujiza wake mkubwa ni Qur'ani ambayo imewashinda nguli wote wa fasihi duniani kuleta mfano wake, na mpaka leo hii bado imeendelea kuwapa changamoto viumbe wote kuileta hata Sura moja tu fupi mfano wake! Na Allah - Mtukufu Amekwishasema kwamba hawataweza kama Aya za Qur'ani zifuatazo zinavyobainisha;

"Na kama nyinyi (Makafiri) mkiwa na shaka na yale ambayo Sisi Tumeteremsha kwa mja Wetu (yaani hii Qur'ani), basi, leteni Sura moja tu mfano wake (kwa balagha na maudhui) na waiteni mashahidi wenu nyinyi (yaani miungu ya bandia mnayoiabudu) kinyume na Allah - Mtukufu (ili ikusaidieni) kama nyinyi ni wakweli (kuwa Mtume-Swallallahu alayhi wasallama ameitunga mwenyewe). Na kama nyinyi hamkufanya (hivyo) na kamwe nyinyi hamtofanya, basi, uogopeni Moto ambao fueli yake (yaani vya

kuuwashia) ni watu na mawe, ulioandaliwa kwa ajili ya wale waliyo makafiri." [Suuratul Baqarah, Q2:23-24].

Muujiza wa pili ni kupasuka kwa mwezi wakati washirikina wa Makka walipompa mtihani wa kufanya hivyo na kisha ukarejea katika hali yake kama Qur'ani inavyobainisha;

"Kimekaribia Kiyama na umepasuka mwezi (vipande viwili kama makafiri walivyoomba). Na kama wao wakiona muujiza wowote ule wao hupuuza na kusema; "(Huu) ni uchawi tu wa kupita." [Suuratul Qamar, Q54:1-2].

Muujiza wa tatu ni kutakaswa kwake na vijiwe vya changarawe katika vidole vyake.

Muujiza wake mwingine ni kuuita mti kutoka mahali pake na ukaja alipokuwa na kisha ukarudi mahali ulipokua wakati bedui mmoja (Mwarabu wa mashambani) alipomuomba Mtume - Rehema na amani ya Allah iwe juu yake amuonyeshe ishara za Utume wake, Mtume akauamrisha mti huo kuja kwake na kisha kurudi sehemu yake.

Muujiza wake mwingine ni pale aliposhika chuchu za maziwa ya mbuzi ambae hakuwa anatoa maziwa yoyote akazifuta kisha akakamua maziwa yakatoka

ya kutosha, akanywa na akampa rafiki yake Sayyidina Abu Bakr - Radhiyallaahu anhu naye akanywa.

Wakati mmoja Sayyidina Ally - Radhiyallaahu anhu alipata kuugua macho, basi Mtume - Rehema na amani ya Allah iwe juu yake akaelekeza aletwe mbele yake na alipofika yeye akamtemea kidogo machoni mwake na akapona ugonjwa wake wakati huo huo.

Na siku nyingine Swahaba wake mmoja aliumia mguu basi, Mtume wa Allah - Mtukufu - Rehema na amani ya Allah iwe juu yake akaushika na kuufutafuta na ukapona muda huo huo.

Na Yeye-Swallallaahu alayhi wasallama alipata kumuombea Sayyidina Anasi bin Malik - Radhiyallaahu anhu awe na umri mrefu, mali nyingi na watoto wengi, na Allah-Mtukufu Alimbariki katika yote hayo, akapata watoto mia na ishirini, na akawa na shamba la mitende, ambalo alikuwa akivuna mara mbili kwa mwaka, wakati katika hali ya kawaida mitende huzaa mara moja tu kwa mwaka, na yeye akaishi miaka mia moja na ishirini.

Wakati mmoja, mmoja miongoni mwa Maswahaba zake alipata kumlalamikia Mtume-Rehema na amani ya Allah iwe juu yake, juu ya ukame wakati Mtume

akiwa juu ya Mimbari, wakati huo huo Mtume akamuomba Allah-Mtukufu Alete mvua, kwa hakika wakati huo hapakuwa na mawingu ya mvua, lakini mara yakaanza kujikusanya mawingu mengi mfano wa majabali, na hapakupita muda mrefu baada yake mvua nyingi ikanyesha kwa muda wa wiki mzima! Maswahaba wakamlalamikia kuwa mvua imekuwa nyingi mno! Mtume akamuomba Allah-Mtukufu kwa mara ya pili, na mvua ikaacha kunyesha.

Miongoni mwa miujiza ya Mtume-Rehema na amani ya Allah-Mtukufu iwe juu yake, ni kuwalisha Maswahaba walioshiriki vita vya Handaki takribani elfu moja kwa pishi moja ya shairi na mbuzi mmoja, wakala na wakashiba na kisha kuondoka hali ya kuwa chakula bado kipo vile vile bila ya kupungua hata kidogo.

Muujiza mwingine ni pale makafiri wa Makka walipodhamiria kumuua, basi yeye alitoka nyumbani kwake wao wakiwa wameizunguuka, akausomea mchanga na kuwamwagia kisha akaondoka na katu hawakuweza kumuona.

Na muujiza mwingine aliofanya ni wakati alipokuwa njiani akielekea Madina, shujaa mmoja wa Kiarabu aitwae Suraqa Bin Maliki aliamua kumfuata ili kwenda kumuua, basi yeye alipomkaribia, Mtume -

Swallallaahu alayhi wasallama akaomba dua na miguu ya farasi wake ikazama katika ardhi na akawa hawezi kwenda kokote!

Miujiza ya Mtume Muhammad - Rehema na amani ya Allah iwe juu yake ni mingi na yote ilitokea kwa Kutaka Kwake Allah-Mtukufu kwa lengo la kuutia nguvu ukweli wa ujumbe wake.

## Misingi ya Dini ya Kiislam

**1. Kumuamini Allah-Mtukufu:** Hii ni asili ya Dini ya Kiislam, ni imani ya kumuamini Allah-Mtukufu Asiye na mshirika, na kusadiki Uwepo Wake, na kwamba Allah-Mtukufu ndio Muumbaji wa kila kitu na Yeye Peke Yake Ndiye Mwenye Kuendesha barabara ulimwengu na vyote vilivyomo ndani yake, Naye Ndiye Anaestahiki kuabudiwa kwa haki bila ya kushirikishwa na chochote, na kwamba Allah-Mtukufu ni Mwenye sifa zote njema na kamilifu na Ametakasika na kila aina ya upungufu na kwamba hakika Yeye Hafanani na kiumbe chochote kile.

Na kwa yeyote anayeutazama ulimwengu na vyote vilivyo ndani yake kwa jicho la moyoni bila shaka atatambua kwamba haiwezekani kwa vitu vyote hivi kuwa vimezuka tu kwa sababu ya mabadiliko ya nyakati, na kwamba haiwezekani kuwa vimepatikana

tu bila ya Kuwepo kwa Muumbaji wake ambaye ni Allah-Mtukufu.

**2. Kuamini kuwepo kwa Malaika:** Malaika ni viumbe katika ulimwengu wa ghaibu, yaani ulimwengu wa vitu visivyoonekana. Wao wameumbwa kwa lengo la kutekeleza Amri zote za Allah-Mtukufu bila ya kusita na kufanya ibada walizopangiwa tu. Hawahusiki na mambo ya uumbaji wala Si viumbe wa kuabudiwa. Kwa hulka tu Allah-Mtukufu Amewafanya kutokuwa na uwezo wa kuasi Amri Zake.

Muislamu anatakiwa kuamini kuwepo kwao na kwamba wako wengi mno na hakuna anaejua idadi yao isipokuwa Allah-Mtukufu Peke Yake.

Muislamu anatakiwa pia kuamini majina ya wale ambao tumefundishwa majina yao, kama vile: Jibrilu, Malaika aliyekuwa akipeleka Wahyi kwa Manabii na Mitume wote. Ridhwan, Malaika aliye mlinzi wa Pepo. Maliki, Malaika aliye mlinzi wa Moto. Izrailu, Malaika mtoa roho za watu na Mikailu na wengineo wengi. Tunatakiwa pia kuamini sifa zao na matendo yao tuliyofundishwa.

**3. Kuamini Vitabu Vyake:** Muislamu anatakiwa kuamini kwamba Allah-Mtukufu Aliye Mwenye kutakasika na mapungufu yote Aliteremsha Vitabu

kwa baadhi ya Mitume na Manabii Wake, kwa lengo la kubainisha haki kwa nyumati zao. Miongoni mwa Vitabu hivyo ni; Taurati kwa Nabii Musa. Injili kwa Nabii Isa na Zaburi kwa Nabii Daudi. Na kuiamini Qur'ani ambayo Allah-Mtukufu Ameiteremsha kwa Mtume Wake wa mwisho Muhammad-Rehema na amani ya Allah iwe juu yake.

**Qur'an**: Huu ni ujumbe wa Allah-Mtukufu ulioteremshwa mwisho kwa ajili ya wanadamu wote. Na Allah-Mtukufu Hatokubali matendo ya mmoja wetu isipokuwa kwa kufuata kilichokuja ndani ya Qur'ani. Na Qur'ani imeletwa ili kutia nguvu mafundisho ya Vitabu vilivyotangulia na kuvisadikisha. Na ndiyo sababu Allah-Mtukufu Ameahidi Kukihifadhi na Kukilinda, hakitaingia dosari wala mabadiliko mpaka Siku ya Kiyama. Jambo hili ni tofauti na Vitabu vilivyotangulia, ambavyo vimebadilishwa kwa mikono ya waandishi kwa sababu Allah-Mtukufu Hakuwa Amevikusudia kuwa vya kudumu na hivyo Hakuahidi Kuvilinda na Kuvihifadhi kama ilivyo kwa Qur'an, ambayo ndio Ujumbe Wake wa mwisho kwa wanadamu wote.

Qur'an katika muundo wake kilugha, upo katika sura nzuri zaidi, na katika upande wa sheria kuna kanuni kamilifu zaidi ikiwa ni pamoja na mambo ya ibada. Qur'ani imetubainishia baadhi ya mambo ya ghaibu,

yaani ya ulimwengu usioonekana, kama vile Malaika, Majini, Moto, Pepo na kadhalika na imetutajia mambo ambayo hakuna mwanadamu ambaye angeweza kuyajuwa mwenyewe na yaliyo nje kabisa ya upeo wa akili ya mwanadamu.

Qur'an kwa tabia yake imeashiria kwenye mambo ambayo hayakuwa yanafahamika na yeyote katika zama zake isipokuwa zama zilizofuata baada ya Mtume Muhammad-Swallallaahu alayhi wasallama kwa kupanuka kwa elimu. Ndani ya Qur'an mna ishara za kanuni ambazo hazikugunduliwa ila baada ya kutawafu kwa Mtume Muhammad-Rehma na amani ya Allah iwe juu yake - kwa miaka 1400 na baadhi hazijagunduliwa mpaka leo hii.

Qur'ani ni Kitabu ambacho ndani yake Allah-Mtukufu Ameweka changamoto za kutosha kwa wanadamu ili kuwainua kitaaluma na kiroho pia.

Miujiza ya Qur'an bado inaendelea Si kwenye maneno yake tu na wala Si kwa sababu ya kueleza mambo ya ulimwengu wa yale yasiyoonekana, yaani ya ghaibu wala kutajwa kwa sheria tu, bali Qur'an yote kama ilivyo ni muujiza.

**4. Kuwaamini Mitume wa Allah-Mtukufu;** Muislamu anatakiwa kuamini kuwa Allah-Mtukufu Alituma Mitume na Manabii kwa lengo la

kuwatanabahisha wanaadamu umuhimu wa kumuabudu Yeye tu Peke Yake na kuacha kila kinachokwenda kinyume na hilo.

Na kwamba Mitume ni wanadamu walioumbwa na wala hawahusiki katika uumbaji kwa namna yoyote wala wao Si wa kuabudiwa, sifa yao ni kama binadamu wa kawaida ambao wanakula, kunywa, kuugua na kufa.

Ni lazima pia kuamini kwamba Mitume na Manabii ni viumbe bora zaidi kuliko binadamu wengine kwa kuwa Allah-Mtukufu Aliwateua wao na Kuwapa yakini ya kuwepo Kwake na Akawakinga wao dhidi ya kutenda dhambi na Akawahusisha wao tu katika kufikisha ujumbe Wake kwa binadamu wenzao.

Na kuwaamini Mitume ni pamoja na kuamini yote waliyokuja nayo kutoka kwa Allah-Mtukufu kuwa ni kweli. Pamoja na kuamini majina yao kwa wale tuliotajiwa majina yao, na kusadikisha mafundisho yao kwa vitendo na kisha kuifanyia kazi sheria na muongozo ulioletwa na wa mwisho wao, yaani Mtume Muhammad - Rehma na Amani ya Allah - iwe juu yake. Kwani Allah-Mtukufu Hakubali watu kufuata sheria ya Mtume mwingine yeyote zaidi yake katika hizi zama zake.

**5. Kuamini kuwepo kwa Siku ya mwisho;** Ambayo ni Siku ya Kiyama, ambapo Allah-Mtukufu Atawafufua watu wote kwa ajili ya hesabu na malipo kila mmoja kwa mujibu wa matendo yake. Na imeitwa Siku ya mwisho kwa kuwa hakutakuwa na siku nyingine baada yake! Siku hiyo watu wa Peponi watapelekwa kwenye makazi yao ya milele na watu wa Motoni nao watapelekwa kwenye makazi yao ya milele, isipokuwa wale ambao Allah-Mtukufu Huruma Yake Atawasamehe baadaye na Kuwaingiza Peponi.

Maana ya kuiamini Siku ya mwisho ni kusadiki bila ya shaka yoyote juu ya kuja kwake, na kujiandaa kwa ajili yake, na hilo linakusanya mambo matatu;

a) Kuamini kufufuliwa kwa watu waliokufa wakati Allah-Mtukufu Atakapowafufua watu wote kutokea wa mwanzo mpaka wa mwisho wao, wakiwa kama walivyozaliwa.

b) Kuamini kuwepo kwa kuhesabiwa, ambapo Allah-Mtukufu Atamuhesabu kila mtu kwa matendo yake ya hapa duniani, na kisha Yeye Amlipe kila mmoja kwa mujibu wa matendo yake! Yule aliyeamini na kutenda mema Amlipe Pepo na yule aliyekufuru na kutenda maovu Amlipe Moto.

Hesabu na malipo ni kwa hekima ya Allah-Mtukufu kwa waja wake, kwani Allah-Mtukufu Aliteremsha Vitabu na kutuma Mitume ili Kuwabainishia watu njia za heri na shari, na Akawajibisha kwa wanaadamu kumuabudu na kumtii Yeye tu Peke Yake.

Na binadamu wako katika makundi mawili, kundi la waumini na wengine ni makafiri, basi, haiwezekani kwa Uadilifu wa Allah-Mtukufu na Hekima Yake makundi yote yawe sawa. Allah-Mtukufu Aliyetakasika na mapungufu yote Amesema ndani ya Qur'an; "Basi, hivi, yule ambaye ni muumini ni kama yule aliye fasiki? Katu wao hawako sawa. Ama kwa wale ambao wameamini na wakafanya matendo mema, wana wao mabustani ya *Ma'awa* kama takrima kwa sababu ya yale (mema) waliyokuwa wanafanya. Na ama wale ambao wamekufuru, basi, marejeo yao ni Moto. Kila pale wao watakapotaka kutoka humo watarejeshwa katikao na wataambiwa; "Onjeni adhabu ya Moto ambayo nyinyi mlikuwa mnaipinga."

c) Kuamini kuwepo kwa Pepo na Moto, na kwamba hayo ni makazi ya kudumu kwa waja. Pepo ni mabustani ya neema ambayo Allah-Mtukufu Ameyaandaa kwa ajili ya waumini wacha Mungu, ambao waliyoamini yale ambayo Allah-Mtukufu

Aliwajibisha kwao, wakawa imara katika kumtii Allah-Mtukufu na Mtume Wake-Swallallaahu alayhi wasallama, wakafanya ibada zao kwa moyo mkunjufu na Ikhlasi na wakamfuata Mtume wake. Watu wa Peponi watakua na madaraja tofauti, na jambo hilo ni kwa sababu ya kutofautiana kwao katika matendo mema.

Na Motoni ni makazi ya adhabu ambayo Allah-Mtukufu Ameyaandaa kwa ajili ya wale makafiri ambao waliyakanusha na kuyapinga mafundisho ya Mitume Wake. Nao pia watakuwa na madaraja tofauti, na jambo hilo ni kwa sababu ya kutofautiana kwao katika matendo yao mabaya.

**6. Kuamini Qadari;** Jambo hili ni moja katika nguzo za imani. Ni lazima mwanaadamu aamini kwa hakika kwamba kila kitu Ki katika Ujuzi wa Allah-Mtukufu, kilichopita, kilichopo na kinachokuja, kile Anachotaka Allah-Mtukufu kitakuwa na kile Asichotaka Yeye katu hakiwezi kutokea, na kwamba hakitokei chochote kile ulimwenguni, hata kuanguka kwa jani kutoka katika mti ila kwa Kujua Kwake na Kutaka Kwake.

# Ibada katika Uislamu

Sharti la ibada yoyote ya mja kukubalika mbele ya Allah-Mtukufu ni kwanza mtu kuwa Muislamu na pili itekelezwe kwa Ikhlasi, yaani kwa kutafuta Radhi Yake Yeye Allah-Subhaanahu wa taala na ifuate utaratibu aliokuja nao Mtume wa Allah-Mtukufu-Rehma na amani ya Allah iwe juu yake.

Swala kwa mfano, hii ni ibada ambayo haitekelezwi ila kwa kumuelekea Allah-Mtukufu, na haiwezi kuwa sahihi isipokuwa itekelezwe kwa kufuata utaratibu alioubainisha Mtume wa Allah-Mtukufu - Rehma na Amani ya Allah iwe juu yake.

Na jambo hili lina sababu zake, ambazo ni;

Allah-Mtukufu Ameamrisha ibada zote zitekelezwe kwa Ikhlasi ya kuabudiwa Yeye tu Peke Yake, kuabudu kitu kingine pamoja na Allah-Mtukufu ni ushirikina. Allah-Mtukufu Anasema:
"Na mumuabudu Allah-Mtukufu tu (Peke Yake) na katu nyinyi msishirikishe pamoja Naye chochote." [Suurat Nisa'i, Q4: 36].

1. Allah-Mtukufu Aliye Mwenye Kutakasika na mapungufu yote Ndiye Aliyeweka sheria, kwa hiyo ni haki Yake Peke Yake na yeyote atakayeabudu kinyume na sheria Zake huyo atakuwa

amemshirikisha Allah-Mtukufu katika suala la uwekaji sheria.

2. Allah-Mtukufu Ametukamilishia Dini, hivyo yeyote ataeleta ibada yake, huyu atakuwa ameituhumu Dini kuwa yenye mapungufu.
3. Lau ingekuwa inafaa kwa kila binadamu kufanya ibada atakavyo kwa muundo autakao, basi kila mtu angekuwa na utaratibu wake mwenyewe wa kufanya ibada, kwa kule kutofautiana tabia na mitazamo ya watu.

## NGUZO ZA UISLAMU

Nguzo za Uislamu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna ni tano:

1.Kushuhudia kwamba hapana Mola Apasaye kuabudiwa kwa haki ila Allah-Mtukufu na hakika Muhammad ni Mtume Wake.
2. Kusimamisha Swala.
3. Kulipa Zaka.
4. Kufunga mwezi mtukufu wa Ramadhani.
5. Kwenda Kuhiji katika Nyumba Tukufu ya Allah-Mtukufu.

# Maana ya Nguzo za Uislamu

1. Kushuhudia kwamba hapana Apasaye kuabudiwa kwa haki ila Allah-Mtukufu na hakika Muhammad ni Mtume Wake.

Maana ya Shahada hii ni kushuhudia kwa kuitakidi bila ya kuwa na shaka kwa kukiri moyoni na kutamka kwa ulimi, kwamba Mwenye kustahiki kuabudiwa kwa haki ni Allah-Mtukufu tu Peke Yake na wala hana mshirika na kushuhudia kwamba Muhammad ni Mtume, yaani mfikishaji ujumbe wa Allah-Mtukufu kwa wanadamu wote pamoja na majini.

Uislamu wa mtu yeyote au matendo yake mema hayatakubaliwa ila kwa Ikhlasi na kutafuta Radhi ya Allah-Mtukufu na kumtii Mtume Wake Muhammad - Rehma na Amani ya Allah iwe juu yake.

Maana ya; Hapana Mola Apasaye kuabudiwa kwa haki ila Allah-Mtukufu, ni mtu kutamka na kuitakidi kuwa Allah-Mtukufu Ndiye Mwenye Haki ya kuabudiwa bila ya kushirikishwa na chochote na kutamka na kuitakidi hivyo hakutoshi kama hakuambatani na matendo yanayofuata maamrisho ya Allah-Mtukufu.

Maana ya, Muhammad ni Mtume wa Allah-Mtukufu ni kumtii kwa aliyoamrisha, kuyasadikisha aliyoyaeleza

kwa vitendo, na kujiepusha na yote aliyoyakataza na kuyakemea.

2. Kusimamisha Swala, ni kuswali Swala zote za faradhi za kila siku kwa wakati na kwa jamaa, yaani swala ya Alfajiri, Adhuhuri, Alasiri, Maghribi na Ishaa.

3. Kulipa Zaka, ni kutoa kiwango maalum cha mali, mifugo, matunda au nafaka ikiwa ni pamoja na kutokana na thamani ya vito vya thamani ambavyo mtu anamiliki kuwapa wanaostahiki, ambao ni pamoja na masikini na wenye mahitaji wengine kama Qur'ani inavyobainisha:

"Kwa hakika Zaka ni kwa ajili ya masikini na wahitaji na wale wenye kuifanyia kazi na kwa kuzoesha nyoyo zao (watu wanaosilimu katika Uislamu) na kwa kukomboa mateka (au watumwa) na kwa wale wenye madeni au kwa matumizi katika misingi ya Dini ya Allah-Mtukufu na kwa wasafiri (walio kwama). Ni wajibu (uliowekwa) na Allah-Mtukufu. Na daima Allah-Mtukufu ni Mjua-yote, Mwenye Hekima.

Na baadhi ya Aya zinazoeleza kuhusu Swala na Zaka ni kama zifuatazo; "Na Utuandikie sisi mema katika dunia hii na huko Akhera kwani kwa hakika sisi tumetubu Kwako Wewe. Yeye (Allah-Mtukufu) Akasema; "Adhabu yangu Mimi Humpatisha yeyote

Ninayemtaka na Huruma Yangu Mimi imekienea kila kitu (duniani). Basi, Mimi Nitaithibitisha Huruma hiyo (Akhera) kwa wale tu wanaojiwajibisha kumcha (Allah-Mtukufu) na hulipa zaka na wale wanaoziamini Aya Zetu Sisi." [Al-A'raf, Q7:156].

"Basi, waumini wanaume na waumini wanawake baadhi yao ni wandani wa wengine. Wao huamrishana yaliyo mema na hukatazana yale mabaya na hustawisha Swala na hulipa Zaka na humtii Allah-Mtukufu na Mtume Wake *(Swalallahu alayhi wasallama)*. Hao ndio ambao Allah-Mtukufu Atawarehemu wao. Kwani kwa hakika Allah-Mtukufu daima ni Mshinda yote, Mwenye Hekima. [At-Tawba, Q9:71].

"(Ewe Mtume - *Swalallahu alayhi wasallama*!) Chukua kutoka katika mali zao Zaka ambayo kwayo wewe utawatwaharisha wao na kuwatakasa (na madhambi) na uwaombee wao dua. Kwani kwa hakika dua yako wewe ni utulivu kwao. Na daima Allah-Mtukufu ni Msikia-yote, Mjua-yote." [At-Tawba, Q9:103].

Kama tunavyoona moja ya faida ya Zaka ni kuitwaharisha nafsi kutokana na madhambi, na ubakhili, pamoja na kukidhi haja za Waislamu wenye

mahitaji, kueneza upendo kati ya waislamu, kujiweka mbali na hasadi, kujenga unyenyekevu na huruma miongoni mwa jamii.

4. Kufunga mwezi mtukufu wa Ramadhani, Ni katika kutii amri ya Allah-Mtukufu na kutakasa nafsi zetu, nako ni kujizuia na vinavyofunguza katika mchana wa Ramadhani. Ni kuacha kula, kunywa, kustarehe na mke/mume na kadhalika kwa kuacha vyote vinavyo funguza, kuanzia kuchomoza kwa Jua mpaka kuzama kwake, kwa muda wa mwezi mzima, kama ibada maalumu kwa ajili ya Allah-Mtukufu.

Na katika faida ya Swaumu ni pamoja na: kuitakasa nafsi, kuizoesha kuacha vinavyopendeza, kwa lengo la kupata Radhi ya Allah-Mtukufu. Na kuizoesha nafsi subira, jambo la subira na uvumilivu wa hali ngumu.

Na faida nyingine ni kukuza Ikhlasi katika kutenda kwa ajili ya Allah-Mtukufu, kujenga tabia ya uaminifu, kujizoeza kufahamu hali za watu masikini na kuutengeneza mwili kuwa na afya njema.

5. Kwenda kuhiji katika Nyumba ya Allah-Mtukufu, nako ni katika ibada ya Allah-Mtukufu kwa kuikusudia Nyumba Yake Tukufu iliyo Makka kwa lengo la kuadhimisha ishara za Dini ya Allah -Mtukufu mara moja tu katika uhai wa mtu, kwa mwenye uwezo.

“Na itangaze kwa watu Hija, wao watakujia wewe hali ya kuwa wenye kutembea kwa miguu na (wenye kupanda) juu ya kila ngamia mwenye kukonda (kwa ajili ya uchovu wa safari na katika vipando vingine mbalimbali) wao watakuja kutoka kila njia ya mbali.” [Q22:27].

## Baadhi ya Sifa za Dini ya Kiislamu.

Uislamu ni Dini ambayo Allah-Mtukufu Ameichagua kwa ajili ya watu wote. Ni dini ambayo inafaa kwa kila zama na mahali popote. Haijaacha jambo la heri ila imelielezea na kulihimiza kufanywa kwake na haikuacha jambo la shari ila imelitahadharisha. Na kamwe wanadamu hawawezi kupata raha wala kuishi maisha yenye utulivu ila kwa kuishi kwa mujibu wa muongozo ulioletwa na Uislamu! Kwa hakika sifa maalum katika Uislamu kamwe haziwezi kupatikana kwenye Dini zingine.

Na baadhi ya sifa maalum katika Uislamu ambazo watu wanazihitajia zaidi ni kama zifuatazo;

Uislamu ni Dini iliyotoka kwa Allah-Mtukufu, na Allah-Mtukufu Ndiye Anayejuwa mambo yenye maslahi kwa waja wake, kama Anavyobainisha ndani ya Qur’ani; “Hivi, Asijue Yule Aliyeumba huku daima Yeye Ndiye Mwenye udiriki wa ndani kabisa

usiyomithilika (katika Kujua Kwake), Aliye Muelewa-yote?." [Al-mulk, Q67:14].
Uislamu ndio Dini pekee inayobainisha mwanzo wa mwanadamu mpaka mwisho wake, na sababu ya kuumbwa kwake. Na umemuwekea wazi huyo mtu njia anayowajibika kuifuata kwenye maisha haya ya dunia, na umemuwekea wazi pia mambo ambayo anapaswa kuwa na hadhari nayo na kujiepusha nayo.

Ndani ya Qur'ani Allah-Mtukufu Anasema; "Enyi watu! Mjiwajibishe kumcha Mola wenu nyinyi Yule Ambaye Amekuumbeni nyinyi kutokana na nafsi moja na Akaumba kutokana nayo mkewe na Akaeneza kutokana na wao wawili wanaume wengi na wanawake (wengi)" [An-Nisa'i, Q4:1],

Na Amesema tena; "Kutokana nayo (hiyo ardhi) Sisi Tumekuumbeni nyinyi na katikayo Sisi Hukurejesheni nyinyi (kwa kuzikwa baada ya kufa kwenu) na kutokana nayo Sisi Tutakutoeni nyinyi (kwa ufufuo) mara nyingine." [Twaha, Q20:55], Na Amesema tena; "Na Mimi Sikuumba majini na watu ila wao wapate kuniabudu Mimi tu." [Adh-dhariyat, Q51:56], Na katika Sura nyingine Allah-Mtukufu Amesema; "Leo hii Mimi Nimekukamilishieni nyinyi Dini yenu na Nimetimiza Neema Zangu juu yenu nyinyi na

Nimeridhia kwenu nyinyi Uislamu kuwa Dini.” [Al-maida, Q5: 3].

Ni Dini inayoendana na maumbile ya binadamu, kwani haipingani na umbo ambalo Allah-Mtukufu Amemuumba mwanadamu kwalo, kama Allah-Mtukufu Aliyetakasika na mapungufu Anavyobainisha ndani ya Qur’ani; “Kuumba kwa Allah-Mtukufu kule ambako Yeye Amewaumba watu juu yake. Katu hapana mabadiliko katika Uumbaji wa Allah-Mtukufu (yaani Dini Yake).” [Ar-Rum, Q30:30].

Ni Dini inayochangamsha akili na kumuamrisha mwanadamu kutumia akili yake vizuri, inapinga ujinga na kuiga mambo ovyo bila ya kuwa na elimu nayo, kama Allah-Mtukufu Anavyosema; “Sema (ewe Mtume-*Swalallahu alayhi wasallama*); Hivi! Wako sawa wale ambao wanajuwa na wale ambao katu hawajui?” [Az-Zumar, Q39:9]. Na katika Sura nyingine Allah-Mtukufu Anasema; “Kwa hakika mna katika uumbaji wa mbingu na ardhi na kupishana kwa usiku na mchana ushahidi (wa Uwezo wa Allah-Mtukufu) kwa wale wenye akili wanaotafakari. Wale ambao humdhukuru Allah-Mtukufu wakiwa wima au wamekaa au wenye kulalia mbavu zao na wakatafakari kuhusu uumbaji wa mbingu na ardhi (na wakasema); “Ee Mola wetu! Wewe Hukuviumba

hivi bure. Utakasifu Wako Wewe, basi, Tuokoe sisi na adhabu ya Moto." [Aal-Imran, Q3:190-191].

1. Uislamu ni itikadi na sheria na umekamilika katika vyote viwili! Si Dini ya kufikiri ni Dini ya vitendo katika maisha yote ya mwanadamu.

2. Ni Dini yenye kuzingatia hisia za binadamu na kuzielekeza kwenye njia iliyonyooka na sahihi iliyo ya haki ni katika nyenzo za kujenga na si za kubomoa.

Ni Dini inayohimiza uadilifu kwa kila mtu, bila ya kujali kuwa ni rafiki au adui, jamaa wa karibu au wa mbali. Ndani ya Qur'ani Allah-Mtukufu Amesema; "Kwa hakika Allah-Mtukufu Anaamrisha uadilifu na ihsani na kuwapa ndugu (wanapokuwa na shida) na Yeye Anakataza machafu (ya zinaa) na mabaya (ya ukafiri na maasi) na kufanya vibaya (juu ya watu). Yeye Anakuwaidhini nyinyi ili nyinyi mpate kuonyeka." [An-Nahli, Q16:90]. Na Amesema tena; "Na pale nyinyi mnaposema, basi, kuweni waadilifu hata kama ni (dhidi ya) ndugu." [Al-An-Aam, Q6:152]. Na katika Sura nyingine Amesema; "Ee, wale ambao wameamini! Kuweni imara kwa ajili ya Allah-Mtukufu kama mashahidi kwa uadilifu. Na katu zisikuzuwieni nyinyi chuki kwa watu kwamba nyinyi

msifanye uadilifu. Fanyeni uadilifu huko (kufanya uadilifu) ni karibu zaidi ya ucha Mungu." [Al-Maida, Q5:8].

Uislam ni Dini inayojenga udugu wa kweli miongoni mwa jamii, kimsingi Waislamu wote ni ndugu katika Dini, hawatenganishwi na miji, utaifa na rangi. Na wala Uislamu hauruhusu ubinafsi kwa utaifa, rangi au nasaba ya kifamilia! Kipimo cha ubora kwa Muislamu mbele ya Allah-Mtukufu ni taqwa, yaani ucha Mungu. Allah-Mtukufu Amesema; "Enyi watu! Kwa hakika Sisi Tumekuumbeni nyinyi kutokana na mwanaume mmoja na mwanamke mmoja (yaani Nabii Adamu na bibi Hawa) na Tumekufanyeni nyinyi kuwa mataifa mbalimbali na makabila ili nyinyi mpate kujuana (katu Si kwa ajili ya nyinyi kushindana). Kwa hakika mtukufu wenu nyinyi mbele ya Allah-Mtukufu ni yule aliye mwema zaidi kati yenu." [Al'Hujuraat, Q49:13]

Uislam ni Dini inayohimiza watu kutafuta elimu, na kuwaahidi wao ujira mkubwa kwa jambo hilo, ndani ya Qur'ani Allah-Mtukufu Anasema; "Na pale nyinyi mnapoambiwa inukeni (ili mkaswali), basi, inukeni, Allah-Mtukufu Atawainua, wale ambao wameamini miongoni mwenu nyinyi na wale ambao wamepewa elimu, madaraja." [Al-Mujaadala, Q58:11].

Na katika Sura nyingine Allah-Mtukufu Anasema; "Je wanaweza kuwa sawa wale wanaojua na wale wasiojua?" [Az-Zumar, Q39:9], na Mtume wa Allah-Mtukufu-Rehma na amani ya Allah iwe juu yake amesema; *"Kutafuta elimu ni faradhi (yaani ni lazima) kwa kila Muislamu."*

Allah-Mtukufu Amechukua dhamana kwamba kila atakayeishi kwa kufuata muongozo Wake ulioletwa kwetu kupitia kwa Mtume Muhammad-*Swallallaahu alayhi wasallama* na kuufanyia kazi Uislamu kama unavyostahiki kufanyiwa, basi bila shaka yeye ataishi maisha mazuri na ya heshima, ni mamoja iwe ni kwa mtu mmoja mmoja au jamii kwa ujumla wake. Ndani ya Qur'ani Allah-Mtukufu Amesema; "Allah-Mtukufu Amewaahidi wale ambao wameamini miongoni mwenu nyinyi na wakafanya matendo mazuri kwamba hakika Yeye Atawafanya wao kuwa Makhalifa (yaani viongozi) katika ardhi kama vile Alivyowafanya kuwa Makhalifa wale wa hapo kabla yao na kwamba Yeye Atawaimarishia wao Dini yao ambayo Yeye Amieridhia kwao (yaani Uislamu) na kwamba hakika Yeye Atawabadilishia wao baada ya hofu yao salama. Kwani wao huniabudu Mimi tu katu wao hawashirikishi kitu pamoja Nami. Lakini yeyote atakayekufuru baada ya hayo, basi, hao wewe ndiyo wale waliyo mafasiki." [An-Nur, Q:55].

Na katika Sura nyingine Amesema; "Yeyote atakayefanya mema awe mwanaume au mwanamke huku yeye ni muumini, basi, kwa hakika Sisi Tutamfanya yeye kuishi maisha mzuri. Na kwa hakika Sisi Tutawajaza wao ujira wao kwa mujibu wa mazuri waliyokuwa wanafanya." [An-Nahli, Q16: 97].

Uislamu ni Dini ya upendo na ya kijamii, yenye kuhimiza kusaidiana na kuhurumiana, Mtume-Rehma na amani ya Allah iwe juu yake amesema; *"Mfano wa waumini katika kupendana, kufanyiana upole na kuoneana kwao huruma ni sawa na mwili mmoja, kiungo kimoja kikihisi maumivu husababisha mwili mzima kupata homa na kukesha."* Na amesema tena; *"Wale wenye kuwahurumia watu, nao watahurumiwa na Allah-Mtukufu, waoneeni huruma waliyo ardhini ili muonewe huruma na Aliye mbinguni."* Na amesema tena; *"Hawi muumini wa kweli mmoja wenu nyinyi mpaka yeye ampendelee ndugu yake kile anachokipendea nafsi yake."*

3. Uislamu ni Dini ya jitihada na kujituma, Mtume-*Swallallaahu alayhi wasallama* amesema; *"Muumini mwenye nguvu ni bora zaidi na mwenye kupendwa zaidi na Allah-Mtukufu kuliko muumini dhaifu, pupia lenye manufaa kwako wewe wala usishindwe na*

*ukipatwa na lolote wewe, 'Usiseme; Lau ningefanya kadhaa wa kadhaa basi, ingekuwa kadhaa wa kadhaa, bali wewe sema: Allah-Mtukufu Ndiye Aliyekadiria na Akitakacho Yeye ndio huwa."*

Uislamu ni Dini kamili isiyo na kasoro yoyote, na Kitabu chake, yaani Qur'ani ndio bora ya Vitabu vyote kama Allah-Mtukufu Anavyosema; "Hivi wao hawatafakari kuhusu hii Qur'ani! Lau ingekuwa ni kutoka kwa asiyekuwa Allah-Mtukufu kwa hakika wangalikuta ndani yake makosa mengi." [An'Nisa'i, Q4:82].

4. Uislamu ni Dini iliyo wazi na nyepesi kufahamika kwa kila mtu.

5. Uislamu uko wazi kwa kila anaetaka kuingia na kuujua.

Uislamu unahimiza tabia njema na matendo mema, Allah-Mtukufu Anasema; "Chukua ule wepesi (katika tabia za watu wala usizipekuepekue) na uamrishe yaliyo mema na uwapuuze (watu) waliyo wajinga." [Al-A'raf, Q7:199]. Na katika Sura nyingine Allah-Mtukufu Amesema; "Na katu hayako sawa (matendo) mazuri na yale yaliyo mabaya. Ondoa (jambo baya) kwa lile lililo zuri, basi, tahamaki! Yule

ambaye kulikuwa kati yako wewe na yeye uadui anakua kana kwamba ni rafiki wa kukutetea wewe." [Fuswilat, Q41:34].

Na Mtume-Rehma na amani ya Allah iwe juu yake amesema; *"Jambo litakalowaingiza watu wengi Peponi ni taqwa, yaani ucha Mungu na tabia njema."* Na katika hadithi nyingine amesema; *"Mkamilifu wa watu kiimani ni yule aliye mzuri wao zaidi kitabia."* Na akasema tena; *"Anayependwa zaidi na Allah-Mtukufu katika watu ni yule mwenye kuwanufaisha wenzie, na kitendo kinachopendwa zaidi na Allah-Mtukufu ni furaha unayompa Muislamu mwenzako, au kumuondolea yeye shida au kumlipia deni au kumuondolea njaa. Na kwenda kumaliza shida ya ndugu yangu Muislamu ni jambo linalopendeza zaidi kwangu mimi kuliko kukaa itikafu Msikitini kwa mwezi mzima."*

Uislamu ni Dini yenye kuhifadhi akili na hiyo ni moja ya sababu iliyoufanya ukaharamisha pombe na madawa mengine ya kulevya, na kila kinachomfanya mtu apoteze akili zake na kudumaza nafsi. Ndani ya Qur'ani Allah-Mtukufu Amesema; "Na katu nyinyi msiue nafsi zenu, kwani kwa hakika Allah-Mtukufu daima kwenu nyinyi Yu Mwenye Huruma." [An-Nisai, Q4:29]

6. Uislamu ni Dini inayohifadhi mali na ndio sababu unahimiza uaminifu kwa kuwasifu watu waaminifu na kuwaahidi wao maisha mazuri hapa duniani na kwenda kuingia Peponi kesho Akhera. Uislamu umeharamisha wizi na kutoa adhabu kali ya mfano hapa duniani kwa atakaefanya hivyo, ili watu wakome kuiba mali za watu na kuwatia hofu.

6. Uislamu ni Dini inayohifadhi nafsi, na ndio sababu ukaharamisha kuua na kuweka adhabu ya kifo kwa muuaji au kulipa fidia! Wauaji wa watu wana adhabu ya milele Motoni. Kwa sababu hiyo kuna matukio machache zaidi ya mauaji katika nchi zenye Waisilamu wengi ambazo zinafanyia kazi sheria hizi. Ni ukweli uliyo wazi kwamba kama mtu atafahamu kuwa akiua mtu na yeye atauawa, wengi watajizuia kufanya hivyo na watu wataishi kwa amani na furaha.

Uislam ni Dini inayohifadhi afya, ndani ya Qur'ani Allah-Mtukufu Amesema; "Enyi wanadamu! Chukueni mapambo yenu katika kila wakati wa swala na kutufu na kuleni na kunyweni na katu nyinyi msifanye israfu, kwani kwa hakika (Allah-Mtukufu) katu Yeye

Hawapendi wale waliyo wabadhirifu." [Al-A'raf, Q7:31]

Na baadhi ya wanazuoni wanasema kuwa Aya hii imekusanya maelekezo mengi yenye manufaa hasa kiafya na jambo hilo ni kwamba kiasi katika kula na kunywa ni katika mambo yanayojenga afya njema."

Kimsingi Uislam umeelekeza njia kadha za kujenga afya njema kwa kuharamisha pombe na aina zote za madawa ya kulevya, kwa madhara ya pombe na madawa ya kulevya yako wazi kwa kila mtu. Na Uislamu umeharamisha pia zinaa na liwaati ambayo ni mambo yanayochangia kwa kiasi kikubwa katika kuenea kwa magonjwa ya zinaa kama kaswende, gonoria, malengelenge na UKIMWI.

Uislamu haujampa binadamu uhuru usio na mipaka katika kuuza na kununua kwake, katika kujieleza kwake na katika mahusiano yake ya kijamii na watu wengine. Ipo mipaka iliyowekwa na Allah-Mtukufu na hakuna mtu anayeruhusiwa kuivuka na miongoni mwa mipaka hiyo ni wizi, ulaghai, ufisadi, udanganyifu na uharibifu katika ardhi.

Katika Uislamu mwanadamu yuko huru kutumia vitu vizuri vilivyo vya halali kwa mujibu wa sheria, katika

vyakula, vinywaji, manukato na mavazi, na kadhalika bila ya madhara kwake mwenyewe au jamii inayomzunguuka.

## Mambo Mazuri Yanayo Himizwa na Uislamu

Uislamu ni Dini iliyokusudia kumfundisha binadamu ustaarabu mzuri wa kuishi kama mtu binafsi na kijamii kwa upana wake! Uislamu umefundisha mambo yote ambayo mwanadamu anahitaji ili kuweza kuishi kwa amani na furaha katika hii dunia na kesho Akhera.

Miongoni mwa mengi tunayoweza kuyapata kwa kutazama mambo tunayoamrishwa kufanya na yale tunayokatazwa na Allah-Mtukufu ni kama ifuatavyo:

## Matendo tunayoamrishwa kufanya.

1) Uislamu unaamrisha matendo yanayoinua heshima za watu kwa kujiepusha na yale yanayotweza heshima zao na kumtukuza Allah-Mtukufu na Mtume Wake kama inavyostahiki kuwatukuza.

2) Uislamu unaamrisha kutumia akili na viungo kwa kufanya matendo yenye tija nzuri kijamii na kibinafsi pia na yenye manufaa duniani na Akhera.
3) Uislamu unaamrisha Ikhlasi katika ibada ya Allah-Mtukufu na uadilifu katika matendo.
4) Uislamu unahimiza kusaidia wenye shida na wahitaji wengine ikiwa ni pamoja na mayatima ndani ya jamii.
5) Uislamu unaamrisha kuwatembelea wagonjwa, kusindikiza Jeneza, kuzuru Makaburi na kuwaombea Dua Waislamu waliozikwa katika makaburi hayo.
6) Uislamu unaamrisha kuwafanyia watu wema na kutowadhulumu wao kwa namna yoyote ile. Mtu apende kuwafanyia wengine kile anachopenda yeye kufanyiwa.
7) Uislamu unaamrisha kufanya kazi na kutafuta riziki kwa njia za halali.
8) Uislamu unaamrisha kuwa na huruma kwa viumbe wote na kuwaondolea madhara.

9) Uislamu unaamrisha kuwafanyia wema wazazi wawili, kuunga udugu, kukirimu wageni, majirani na kuwa wapole kwa wanyama tunaowafuga.

10) Uislamu unaamrisha kuwa na muamala mzuri na watu, kati ya mke na mume pamoja na watoto.

11) Uislamu unaamrisha uaminifu, kutekeleza ahadi, kuwa na dhana nzuri juu ya watu, kuwa na fikra chanya na kufanya mambo ya kheri yote kila mtu kwa kwa kadiri ya uwezo wake.

## Mambo tunayokatazwa kufanya.

Na katika mambo mazuri yaliyoletwa na Uislamu ni makatazo yake ili kumzuia mwanadamu kujitumbukiza katika shari za duniani na Akhera.

1) Uislamu umekataza ukafiri na ushirikina wa watu, masanamu na kadhalika.

2) Uislamu umekataza kiburi, chuki, kujiona, husda na kufurahi kwa matatizo ya wengine.

3) Uislamu umekataza dhana mbaya juu ya watu, kupeleleza mambo ya watu, kukata tamaa, ubakhili na kufanya israfu.

4) Uislamu umekataza uvivu, woga wa kupita kiasi, uvivu wa kutofanya kazi, kufanya mambo kwa haraka bila ya kutafakari, lugha chafu, kukosa haya, kukosa subira, uzembe, hasira, kutokuwa na busara pamoja kukasirishwa na mambo yaliyopita

5) Uislamu umekataza ukaidi, kuwa na roho mbaya kiasi cha kutowasaidia wenye shida.

6) Uislamu umekataza kusengenya, umbea, fitina na kuchonganisha watu kwa lengo la kuharibu uhusiano wao.

7) Uislamu umekataza kuongea maneno mengi yasiyokuwa na faida, kutoa siri za watu, kudhalilisha watu na kuwadharau.

8) Uislamu umekataza kulaani watu na kuitana kwa majina mabaya.

9) Uislamu umekaza mijadala isiyokuwa na tija, magomvi, na utani mbaya unaoweza kuleta shari na kucheka kupita kiasi.

10) Uislamu umekataza kukataa kutoa ushahidi, kutoa ushahidi wa uongo, kuwazushia wanawake

wema mambo machafu, kuwasema vibaya watu waliokufa na kuficha elimu.

11) Uislamu umekataza mambo ya kipuuzi, maneno mabaya, kusimanga baada ya kutoa sadaka, na kutoshukuru wanaokufanyia wema.

12) Uislamu umekataza hiyana, vitimbi na kutotekeleza ahadi.

13) Uislamu umekataza kutowaheshimu wazazi, kuvunja udugu, na kupuuza malezi ya watoto.

14) Uislamu umekataza kufuatilia aibu za watu.

15) Uislamu umekataza wanaume kujifananisha na wanawake na wanawake kujifananisha na wanaume.

16) Uislamu umekataza kunywa pombe, kutumia madawa ya kulevya, na kucheza kamari ili kudhibiti ufujaji wa mali.

17) Uislamu umekataza kuzipamba bidhaa kwa viapo vya uongo wakati wa kuziuza, kupunja

katika vipimo, kujipatia mali kwa njia za haramu na kuudhi majirani.

18) Uislamu umekataza wizi, unyang'anyi hiyana kwa wenye kushirikiana, kuchelewesha malipo kwa waliofanya kazi au kutomlipa mtu baada ya kumaliza kazi.

19) Uislamu umekataza ulafi kiasi cha mtu kupata madhara.

20) Uislamu umekataza watu kutengana, kugombana na kufanyiana uadui na umekataza vikali kutengana kwa zaidi ya siku tatu bila ya kupatana.

21) Uislamu umekataza kuwatishia watu kwa silaha na kumpiga mtu bila sababu za kisheria.

22) Uislamu umekataza zinaa, kulawiti, kutazama picha za ngono na kuua nafsi isiyo na hatia.

23) Uislamu umekataza kutoa na kupokea rushwa.

24) Uislamu umekataza kutosaidia wenye kudhulumiwa kwa wenye uwezo wa kusaidia.

25) Umekataza mtu kuingia kwenye nyumba za watu bila idhini ya wahusika na kusikiliza mazungumzo ya watu bila idhini yao.

## SIKU YA MWISHO

Mtu hawezi kuwa muumini wa kweli mpaka kwanza aamini bila ya shaka yoyote kuwepo kwa Siku ya mwisho na yote yanayohusiana nayo, ambapo Allah-Mtukufu Amesema: "Nyinyi hamuamini Siku ambayo itawafanya watoto watokwe na mvi" [Al-Muzammil, Q73:17]. Na katika kuielekea Siku hiyo hatua ya kwanza ni;

Mauti: Ni mwisho wa kila kiumbe hai hapa duniani, ndani ya Qur'ani Allah-Mtukufu Amesema; "Kila nafsi itaonja mauti." [Aal Imran, Q3:185], Na Amesema tena; "Kila kilicho juu ya ardhi kitakufa." [Ar-Rahman, Q55:26]. Na Allah-Mtukufu Akasema kumuambia Nabii Wake-Rehma na amani ya Allah iwe juu yake:- "Kwa hakika wewe utakufa na kwa hakika wao pia watakufa. Kisha kwa hakika Siku ya Kiyama mbele ya Mola wenu mtabishana." [Az-Zumar, Q39:30-31]. Hakuna binadamu yeyote atakaeishi milele duniani, ndani ya Qurani Allah-Mtukufu Amesema; "Na Sisi Hatukujaalia kwa mtu yeyote kabla yako wewe kuishi milele." [Al-Anbiyai, Q21:34], Aya zote hizi

zinaashiria mambo kadhaa, na miongoni mwa hayo ni;

1) Hakika kwamba watu wengi wameghafilika na kifo, pamoja na kwamba kifo ni jambo la hakika kuliko uhai na hakuna atakayekwenda na chochote kaburini mwake isipokuwa matendo yake tu, yakiwa matendo mema yeye atakuwa na furaha na yakiwa matendo mabaya yeye atakuwa na huzuni.

2) Kwamba hakuna binadamu anayejuwa siku yake ya kufa isipokuwa Allah-Mtukufu tu Peke Yake, wala hakuna mtu anayejuwa atafia wapi, kwa sababu hilo ni katika mambo yaliyo nje ya upeo wa binadamu.

3) Kwamba siku ya kifo cha mtu inapofika hakuna wa kuiahirisha. Ndani ya Qur'ani Allah-Mtukufu Amesema; "Na kwa kila umati (kuna) muda (uliopangwa), basi, pale unapowadia muda wao katu hautaakhirishwa kwao saa wala hautaharakishwa kwao." [Al-A'raf, Q7:34].

Kwamba wakati muumini anapofikiwa na kifo, humjia yeye Malakul-mauti, yaani Malaika mtoa roho akiwa katika sura nzuri na rihi nzuri kabisa, akiwa na Malaika wengine wakimbashiria yeye Pepo. Ndani ya

Qur'ani Allah-Mtukufu Anasema; "Kwa hakika wale ambao wamesema; "Mola wetu sisi ni Allah-Mtukufu tu kisha wao wakabaki kwenye njia sahihi iliyo ya haki (yaani Uislamu) Malaika watateremka juu yao (wakati wa kufa kwao, wakisema) katu nyinyi msihofu wala msihuzunike, lakini pokeeni habari njema ya Pepo ambayo nyinyi mliahidiwa." [Fussilat, Q41:30].

Na ama kafiri anapofikwa na kifo humjia yeye Malakul-mauti, yaani Malaika mtoa roho akiwa na sura ya kutisha na harufu mbaya kabisa, akiwa na Malaika wa adhabu wakimpa yeye habari za Moto, Ndani ya Qur'ani Allah-Mtukufu Amesema; "Na lau wewe ungeona pale madhalimu wanapokuwa katika sakarati ya kifo chao na Malaika wakiwanyooshea wao mikono yao (wakisema) zitoeni nafsi zenu, leo hii nyinyi mtalipwa adhabu ya kudhalilisha kwa sababu nyinyi mlikuwa mnasema dhidi ya Allah-Mtukufu mengine badala ya ukweli na kwa Aya Zake nyinyi mlikuwa na kiburi (basi, ungeona jambo kubwa kabisa)." [Al-An'Am, Q6:93].

Wakati wa kifo ukweli hujulikana na mambo yote huwekwa wazi kwa kila mtu, ndani ya Qur'ani Allah-

Mtukufu Amesema; "Hata pale kinapomjia mmoja wao (hao makafiri) kifo (na akaona makazi yake Motoni) yeye husema; "Ee, Mola wangu! Unirejeshe mimi (Duniani). Ili nikafanya mema katika yale ambayo nimeacha nyuma." Hasha! (Hakuna kurejeshwa)! Kwa hakika ni neno tu analosema, hali ya kuwa kuna mbele yao kizuizi mpaka Siku wao watafufuliwa (na wakaadhibiwe kwa sababu ya uasi wao)." [Al-Mu'minun, Q23:99-100],
Kwa hakika Siku hiyo kafiri atatamani arudishwe duniani ili akatende mema lakini wakati huo majuto hayatomsaidia kitu! Ndani ya Qur'ani Allah-Mtukufu Amesema; "Na utawaona wale madhalimu wakati watakapoiona ile adhabu wakisema hivi kuna kwa kurudi njia yoyote?" [Ash-Shura, Q42:44].

**Kaburi**: Ni kituo cha kwanza katika vituo vya Akhera, yeyote atakayeokoka hapo yanayokuja mbele yake yatakuwa mepesi. Na yeyote atakayeadhibiwa hapo yanayokuja mbele yake yatakuwa mazito! Imepokewa kutoka kwa Sayyidina Anas bin Malik-Allah-Mtukufu Amuwie radhi kutoka kwa Nabii wa Allah-Rehma na amani ya Allah iwe juu yake amesema; *"Hakika baada ya mja kuwekwa kaburini mwake na ndugu zake wakaondoka, hakika yeye husikia sauti ya viatu vyao."* Na akasema tena; "*Watamjia yeye Malaika wawili na kukaa naye, kisha*

*watamuuliza yeye; 'Wewe ulikuwa unasema nini kuhusu huyu mtu (wakimkusudia yeye Mtume Muhammad-Swallallaahu alayhi wasallama)?"* Na yeye atasema; "Ama yule muumini yeye atasema; '*Nashuhudia ya kwamba yeye ni mja wa Allah-Mtukufu na Mtume Wake!*" Na yeye akasema tena; "*Hapo yeye ataambiwa; Tazama yaliyokuwa makazi yako Motoni, hakika Allah-Mtukufu Amekubadilishia wewe na kukupa makazi ya Peponi badala yake! Mtume wa Allah - Rehma na amani ya Allah-Mtukufu iwe juu yake akasema; "Yeye ataonyeshwa sehemu zote mbili.'*

Ama mtu aliye kafiri au mnafiki (kwa swali hilo), yeye atasema; "Mimi sijuwi, nilikuwa nasema kama walivyokuwa wakisema watu wengine!" Na hapo ataambiwa; *"Hutajua wala hutasoma!" Kisha atapigwa na kibarango, yaani nyundo ya chuma kati ya masikio yake na atapiga ukelele mmoja ambao utasikika sauti yake na kila kiumbe isipokuwa binadamu na majini."*

Na kurejea kwa roho katika mwili wa binadamu akiwa kaburini ni katika mambo ya Akhera ambayo Allah-Mtukufu Ameyaweka nje ya upeo wa akili ya binadamu. Allah-Mtukufu Anatueleza kwamba mtu hupata neema kaburini mwake kama yeye alikuwa

muumini wa kustahiki neema hiyo! Na mwingine ataadhibiwa kaburini mwake kama yeye ni mwenye kustahili adhabu kama Allah-Mtukufu hajamsamehe.

Ndani ya Qur'ani Allah-Mtukufu Amesema; "Na Moto huonyeshwa kwao asubuhi na jioni. Na Siku ya Kiyama (itasemwa); "Waingizeni watu wa Firauni (pamoja naye) katika adhabu kali kabisa." [Ghafir, Q40:46],

Na Mtume -*Swallallaahu alayhi wasallama* amesema; *"Takeni hifadhi kwa Allah-Mtukufu kutokana na adhabu ya kaburini."*

Akili makini haiwezi kupinga jambo hilo, kwa kuwa kuna mifano mingi tu ya kulithibitisha jambo hilo katika maisha yetu. Maana upo wakati katika njozi mtu anaweza kuona kuwa anaadhibiwa na akapiga kelele na kuomba msaada, hali ya kuwa aliyelala pembeni yake tu hahisi chochote, pamoja na kuwepo kwa tofauti kubwa kabisa kati ya uhai na kifo.

Na adhabu ni kwa roho na mwili kwa pamoja! Mtume wa Allah-Rehma na amani ya Allah- iwe juu yake amesema; *"Hakika kaburi ni kituo cha kwanza katika vituo vya Akhera, mja akiokoka hapo yanayokuja kwake baadaye ni mepesi! Na asipookoka hapo, basi yanayokuja mbele yake ni mazito,"* kwa hivyo

Muislamu anatakiwa kukithirisha kuomba hifadhi kwa Allah-Mtukufu kutokana na adhabu ya kaburi, hasa akiwa kwenye Swala kabla ya kutoa salamu ya kumaliza Swala! Na afanye pia jitihada ya kujiepusha na maasi ambayo ni sababu ya adhabu ya kaburini na motoni!

Na imeitwa adhabu ya kaburini kwa sababu watu wengi hufa na kuzikwa makaburini, ukiachilia mbali wale waliokufa kwa kuzama majini au kuteketezwa kwa moto au kuliwa na wanyama wakali na kadhalika, hawa huwa wanastareheshwa au kuadhibiwa wakiwa *Barzakh* (yaani kituo cha uhai kati ya kifo na kufufuliwa).

Na adhabu za kaburini zipo za aina mbalimbali, ipo ya kupigwa na kibarango, yaani nyundo za chuma au nyenginezo, kama ya kaburi kujazwa giza na kutandikiwa moto au kufunguliwa mlango wa motoni na hivyo kupata joto lake au vitendo vyake vibaya kuumbwa kiumbe mwenye sura mbaya ya kutisha mwenye harufu mbaya kabisa ambaye atakaa nae hapo kaburini, huku adhabu zikiendelea kama atakuwa kafiri au mnafiki. Na kama atakuwa muumini mwenye makosa, yeye ataadhibiwa kiasi cha madhambi yake na huenda ikakoma adhabu hiyo.

Ama muumini aliyetenda mema ya kuweza kumpatisha Radhi ya Allah-Mtukufu kwa hakika yeye atapata neema akiwa kaburini, kaburi yake itapanuliwa na kujazwa nuru! Mlango wa Peponi utafunguliwa kwa ajili yake na atafikiwa na rihi yake nzuri na atatandikiwa tandiko la kutoka Peponi, na matendo yake mema yataumbwa na kuwa kiumbe mwenye sura nzuri ambaye atakuwa anamliwaza hapo kaburini.

Kwa hakika Peponi mna raha zake kama Allah-Mtukufu Anavyobainisha kidogo ndani ya Qur'ani;

"Na wale wenye kutangulia (kwenye heri katika umati wa kila Nabii) wale wenye kutangulia! Hao wewe ndiyo wale wenye kuwekwa karibu (na Rehema ya Allah-Mtukufu). Hali ya kuwa katika mabustani ya neema tele. Kundi kubwa (litakuwa) miongoni mwa wale wa mwanzo (katika kuwaamini Mitume na kuwa karibu nao). Na wachache miongoni mwa wale wa mwisho (yaani wale waliowaamini Mitume baada ya wale wa mwanzo katika umati huu na zile nyumati zilizotangulia). Watakuwa juu ya makochi-kitanda ya kifakhari yenye kufumwa (kwa nyuzi za dhahabu na johari). Hali ya kuwa wenye kuegemea juu yake wenye kutazamana. Watawazunguukia wao (kwa huduma mbalimbali za kudumu) vijana wenye kufanywa wa milele. Na gilasi za pombe toka

chemchemi ya pombe yenye kutiririka (daima). Katu wao hawataumwa vichwa kwayo wala wao hawatarukwa na akili. Na matunda katika yale ambayo wao watachagua. Na nyama za ndege katika zile ambazo wao watatamani. Na (wana wao kwa kujistarehesha) *Hurun'ain*: Wanawali weupe wenye macho meupe pee na weusi, makubwa yaliyo mazuri. Mfano wa Lulu zenye kuhifadhiwa. Malipo kwa mujibu wa yale (matendo mema) ambayo wao walikuwa wanafanya. Katu wao hawatasikia humo machafu wala kupewa dhambi. Isipokuwa neno *Salaman salama*!" Na watu wa kulia ni nani hao watu wa kulia? Watakuwa katika mikunazi isiyo na miba. Na migomba yenye mikungu yenye kupangwa (vizuri) baadhi yake juu ya mingine kutoka chini hadi juu yake. Na kivuli cha kudumu. Na maji yenye kutiririka daima. Na matunda mengi. Katu Si yenye kukatika (kwa msimu) wala yenye kuzuiliwa (kuliwa). Na matandiko ya kifakhari yenye kuinuliwa (juu ya makochi-kitanda). Kwa hakika Sisi Tumewazusha wao (hao *Mahurul'ain* pasi na kuzaliwa) kuwazusha. Na Sisi Tumewafanya wao kuwa bikira (wa kudumu). Wenye kujipendekeza sana (kwa waume zao) waliyo rika moja. Kwa ajili ya watu wa kulia. Ni kundi miongoni mwa wale wa mwanzo. Na kundi miongoni mwa wale wa mwisho (katika umati Muhammad- *Swallallahu alayhi wasallama*). [Q56:10-40]

## Ishara za Kukaribia kwa Kiyama

1. Mwenyezi Mungu Hakuumba huu ulimwengu kwa ajili ya kubaki milele, ni wa muda maalumu uliopangwa Naye na itafika Siku yake ya mwisho!

Siku hiyo ndio inayojulikana kama Siku ya Kiyama ambapo kila kilicho hai kitakufa na baadaye kufufuliwa na Allah-Mtukufu kwa ajili ye hesabu na malipo kwa mujibu wa matendo ya kila mtu. Watakaofuzu wataingizwa Peponi na humo wataishi milele na watakaofeli wataingizwa Motoni na humo wataishi milele.

Ni Siku ambayo haina shaka kutokea kwake, ndani ya Qurani Allah - Mtukufu Anasema; "Kwa hakika Kiyama kinakuja katu hapana shaka katikacho lakini watu wengi katu wao hawakiamini." [Ghafir, Q40:59] Na katika Sura nyingine Allah - Mtukufu Amesema; "Na wanasema wale ambao wamekufuru; "Katu hakitakuja kwetu sisi kile Kiyama." Sema (ewe Mtume-*Swallallahu alayhi wasallama*); "Kwani! Ninaapa kwa Mola wangu mimi hakika kitakujieni nyinyi!" [Saba,' Q34:3]

Ni lini kitatokea ni siri ya Allah-Mtukufu na wala hakuna hata mmoja katika waja Wake aliyepata kujulishwa jambo hilo. Ndani ya Qur'ani Allah-

Mtukufu Anasema; "Wanakuuliza wewe (Mtume-Swallallaahu alayhi wasallama), wale watu (kuhusu) Kiyama (lini kitakuwa?")! Sema; "Kwa hakika kukijua Ku kwa Allah-Mtukufu tu." Na ni kitu gani kitakachokujulisha wewe huenda Kiyama Ki karibu." [Al-Ahzab, Q33:63].

2. Hakitasimama Kiyama ila kwa watu wabaya peke yao, na hilo ni kwamba kabla ya kusimama Kiyama Allah-Mtukufu, Aliye Mwenye Kutakasika na mapungufu yote Atatuma upepo mororo ambao utazitoa roho za waumini wakati ambao Allah-Mtukufu Atataka kuwafisha viumbe Wake na hivyo dunia kufika mwisho wake! Allah-Mtukufu Atamuamrisha Malaika Israfilu kupuliza baragumu na watu wataisikia sauti yake na wote watakufa. Ndani ya Qur'ani Allah-Mtukufu Amesema; "Na litapulizwa lile Baragumu (mpulizo wa kwanza) na watakufa wote waliyo mbinguni na wote waliyo ardhini isipokuwa wale tu ambao Allah-Mtukufu Atataka." [Az-Zumar, Q39:68],

Na hiyo itakuwa Siku ya Ijumaa, kisha baada ya hapo watakufa Malaika wote, hakuna kiumbe kitakachobaki ispokuwa Allah-Mtukufu tu Peke Yake, Aliye Mwenye Kutukuka!

3. Mwili wa kila mwanadamu, baada ya kuzikwa utaliwa na Ardhi isipokuwa kifupa cha asili yake kinachoitwa kifandugu, nacho ni kifupa cha mwisho kabisa katika uti wa mgongo! Ama miili ya Manabii hubaki kama ilivyo Allah-Mtukufu Amezuwiya ardhi kula miili yao! Siku ya kufufuliwa Allah-Mtukufu Atateremsha maji kutoka mbinguni na miili itaota kutoka ardhini.

Pale Allah-Mtukufu Atakapotaka Kuwafufua watu Atamfufua kwanza Israfilu, Malaika mpulizaji wa Baragumu na atapuliza Baragumu hilo kwa mara ya pili na hapo watafufuka viumbe wote na watu watatoka makaburini mwao wakiwa uchi kama walivyoumbwa na Allah-Mtukufu mara ya kwanza, bila ya kutahiriwa! Ndani ya Qur'ani Allah-Mtukufu Amesema; "Na kutapulizwa baragumu (mpulizo wa pili, hapo zirudishwe roho zao kwenye miili yao) wakitahamaki wanatoka makaburini mwao wakielekea kwa mola wao kwa haraka." [Yaa-Siin, Q36:51]. Na wa kwanza kabisa ambaye atatoka kaburini mwake ni Mtume Muhammad - Rehema na amani ya Allah-Mtukufu iwe juu yake. Kisha watu watapelekwa kwenye ardhi ya kukusanyikia na itakuwa ardhi pana iliyotandikwa (tambarare) na litasogezwa jua kuwa karibu na viumbe.

Watu watabaki kwenye ardhi hiyo kwa muda mrefu ambao Allah-Mtukufu Atataka wakisubiri ufafanuzi kati yao na hesabu, kisha Allah-Mtukufu Atatoa idhini ya kulipana kati yao! Halafu *Swiratwa* itawekwa katikati ya moto wa Jahanamu, yaani daraja jembamba kuliko unywele na lenye makali kuliko upanga, hapo watapita watu kulingana na matendo yao, wapo watakaopita kama kupepesa kwa jicho, wengine kama upepo, wengine kama farasi mwenye kasi, wapo watakaopita wakitambaa kwa magoti na mikono yao! Na pembeni ya *Swiratwa* kuna ndoano ya kuwanasia watu na kuwatupa kwenye Moto wa Jahannam! Wengi watakaoangukia humo ni wale makafiri na wale ambao Allah-Mtukufu Atataka katika waumini ambao waliasi duniani.

Makafiri ni wakazi wa Motoni humo wao watabaki milele. Na ama wale waumini waliomuasi Allah-Mtukufu duniani, wao wataadhibiwa Motoni kwa muda ambao Allah-Mtukufu Atataka na kisha watatolewa na kuingizwa Peponi.

Na wale watakaokuwa wamevuka ule Moto kupitia daraja hilo, ambao ni watu wa Peponi watasimama juu ya kizuizi kilichopo kati ya Pepo na Moto kwa namna ambayo kila aliyepata kuchukua haki ya mwenzake atamlipa haki yake wakati huo. Hakuna

atakayeingia Peponi isipokuwa kwanza alipe haki za watu wote anazodaiwa na ndugu zake waislamu!

Basi, pale watu wa Peponi watakapoingia peponi na watu wa motoni kuingia Motoni, kifo kitaletwa katika sura ya kondoo na kuchinjwa kati ya Pepo na Moto, huku watu wa Peponi na Motoni wakitazama, kisha itanadiwa; "Enyi watu wa Peponi nyinyi mtakaa humo milele, wala hamtakufa, na nyinyi watu wa Motoni mtakaa humo milele, wala hamtakufa. Na lau ingekuwa mja anaweza kufa baada ya hapo, basi wangekufa watu Peponi kwa furaha ambayo wameipata! Na lau ingekuwa mja anaweza kufa baada ya hapo, basi wangekufa watu wa Motoni kwa huzuni ambayo wameipata."

## Ukali wa Adhabu ya Moto

Ndani ya Qur'ani Allah-Mtukufu Amesema; "Uogopeni Moto ambao kuni zake ni watu na mawe umeandaliwa kwa wenye kumkanusha Allah-Mtukufu na Mtume wake" [Suuratul Baqarah, Q2:24]. Na Mtume wa Allah-Mtukufu-Rehema na amani ya Allah iwe juu yake - amesema kuwaambia Maswahaba zake; *"Moto wenu huu, (ambao nyinyi mnawasha) ni sehemu moja tu katika sehemu sabini za ukali wa Moto wa Jahannam."* Na wao wakasema: "Tunaapa kwa Jina la Allah-Mtukufu lau ungekuwa na ukali huu

tu ungetosha ee Mtume wa Allah-Mtukufu.' Na yeye akasema tena; *"Hakika Moto huu umezidiwa ukali mara sitini na tisa na zote zina ukali kama huu."*

Moto wa Jahanamu una tabaka saba, na kila tabaka ina adhabu kali kuliko nyingine, Na kila tabaka ina watu wake kutokana na aina ya matendo yao mabaya. Na ndio ikasemwa wanafiki watakuwa katika daraja la chini kabisa Motoni na ndio kwenye adhabu kali kabisa isiyomithilika. Na Adhabu ya Moto kwa makafiri ni ya kudumu daima dawamu. Kila watakapoungua watapewa ngozi nyingine kwa ajili ya kuendelea kwa adhabu, ndani ya Qur'ani Allah-Mtukufu Anasema; "Kwa hakika wale ambao huzikufuru Aya Zetu hivi karibuni Sisi Tutawaingiza wao Motoni (waungue humo) kila pale zinapobabuka ngozi zao Sisi Tutawaba-dilishia wao ngozi zingine ili wao wapate kuionja ile adhabu." [An-Nisai; Q4:56], Na katika Sura nyingine Allah-Mtukufu Amesema; "Na wale ambao wamekufuru kuna kwa ajili yao Moto wa Jahanamu katu hapataamuliwa kwao kwamba wafe (ili wapumzike adhabu) wala adhabu haitapunguzwa kwao. Kama hivyo wewe Sisi Humlipa kila mwingi wa kufuru." [Fatwir, Q35:36]. Na humo mikono yao itafungwa shingoni mwao, ndani ya Qur'ani Allah-Mtukufu Amesema; "Na wewe (Mtume - *Swalallahu alayhi wasallama*) utawaona wale waovu Siku hiyo

wenye kufungwa katika zile pingu. Kanzu zao za lami na utazifunika nyuso zao Moto." [Ibrahim, Q14:49 - 50]. Na katika Sura nyingine ndani ya Qur'ani Allah-Mtukufu Amesema; "Kwa hakika Sisi Tutafunga katika shingo zao pingu na hizo ni hadi videvuni na wana wao vichwa vyenye kuinuliwa (katu wao hawawezi kuviinamisha)." [Q 36:08].

Na chakula cha watu wa motoni ni matunda ya mti wa Zaqqum, ndani ya Qur'ani Allah-Mtukufu Amesema; "Kwa hakika mti wa Zaqqum. Ndio chakula cha wenye dhambi. Kama madini yaliyoyeyushwa, yanachemka ndani ya tumbo. Kama kuchemka kwa maji ya moto.' [Ad-Dukhan, Q44:43-46]. Na Qur'ani inabainisha ukali wa adhabu ya moto, na ukubwa wa neema za Peponi, kwa yaliyokuja kutoka kwa Nabii-Rehema na amani ya Allah-Mtukufu iwe juu yake, yeye amesema; *"Ataletwa yule aliyekuwa na neema za duniyni katika watu wa motoni Siku ya Kiyama na atatazamishwa kwenye moto mara moja, kisha aambiwe; "Ewe mwanadamu hivi wewe umeona heri yoyote? Hivi zilipata kukupitia wewe neema zozote?" Na yeye atasema; "Hapana, ninaapa ee Mola wangu, hazijawahi kunipata mimi neema zozote.'"*

*Halafu ataletwa yule aliyekuwa na maisha mabaya zaidi hapa duniani katika watu wa Peponi na atatazamishwa Peponi mara moja, kisha aambiwe; "Ewe mwanadamu, hivi wewe umeona ubaya wowote? Hivi ziliwahi kukupitia wewe shida zozote?" Na yeye atasema; "Hapana, ninaapa ee Mola wangu haujawahi kunipitia mimi ubaya wowote?"*

Kwa maana hiyo kafiri anapokuwa Motoni atasahau neema na maisha mazuri yote aliyopitia kwa kuzamishwa Motoni mara moja tu! Na muumini atasahau shida zote alizopitia duniani kwa kuingizwa Peponi mara moja tu!

## Pepo na Neema Zake

Pepo ni nyumba nzuri ya kudumu na heshima, Allah-Mtukufu Ameiandaa kwa ajili ya watu Wake waliyo wema, ndani ya Pepo hiyo mna neema ambazo hakuna jicho la mtu lililopata kuona, wala sikio kusikia, na wala kupita katika fikra za mja yeyote! Ndani ya Qur'ani Allah-Mtukufu Amesema; "Na hakuna nafsi inayoyajua yale yaliyofichwa kwa ajili yake ya furaha ya macho kama zawadi kwa yale (mema) waliyokuwa wanafanya." [As-Sajdah, Q32:17],

Na Pepo ina madaraja yanayotofautiana, waumini watakuwa na nafasi zao ndani yake kwa mujibu wa

matendo yao mema. Ndani ya Qur'ani Allah-Mtukufu Amesema; "Allah-Mtukufu Atawainua, wale ambao wameamini miongoni mwenu nyinyi na wale ambao wamepewa elimu, madaraja." [Al-Mujadila, Q 58:11]. Watakula na kunywa humo Peponi kama wanavyotaka. Humo mna maji matamu yasiyobadilika rangi wala ladha yake. Na mito mingine ya maziwa yasiyoharibika ladha yake na mito ya asali iliyo safi, na mito ya pombe safi yenye ladha nzuri kwa wanywaji. Pombe hiyo haiharibu akili wala kuumisha vichwa! Ndani ya Qur'ani Allah-Mtukufu Amesema; "Vitapitishwa miongoni mwao vikombe (vya mvinyo) kutoka chemchemi yenye kutiririka. Mweupe na mtamu kwa wale wenywe kunywa. Hakuna kuumwa na kichwa kutokao wala wao hawatalewa." [As-Swaffat, Q37:45-47]. Na humo wataoa wanawake wa Peponi, Mtume wa Allah-Mtukufu-Rehema na amani ya Allah iwe juu yake amesema; *"Lau mwanamke katika wale wa Peponi angetokea kwa watu walio katika ardhi, basi yeye angeliviangaza vilivyo kati ya mbingu na ardhi, na angevijaza rihi nzuri."*

Na Neema kubwa kuliko zote kwa watu wa Peponi ni kumuona Allah-Mtukufu, Aliye Mwenye Kutakasika. Licha ya Peponi kuwa makazi ya milele na milele ya watu wema, lakini ni mahali patukufu pia na kwa

sababu hiyo watu wa Peponi hawatakuwa wakienda kujisaidia Si haja ndogo wala kubwa, hawatakuwa wakitoa kamasi wala kutema mate humo. Watakuwa na vitana vya dhahabu na jasho lao litakuwa na harufu ya miski. Na neema zote hizi kwao ni za kudumu daima dawamu na wala hazitapungua! Mtume wa Allah - *Swallallaahu alayhi wasallama* - amesema; *"Yeyote atakayeingia Peponi yeye ataneemeka wala hakuna ubaya ndani yake, hazitachakaa nguo zake wala hautamalizika ujana wake."* Na atakaepata ya daraja la chini kabisa katika watu wa Peponi ni yule wa mwisho kutoka Motoni katika wale waumini, hata hivyo hiyo ni bora zaidi kuliko kupata mara kumi ya vitu vya anasa vya duniani.

## Haki za Mwanamke katika Uislamu

Kabla ya kujadili haki za mwanamke katika Uislamu, hatuna budi kwanza tutazame baadhi ya mitazamo na misimamo ya nyumati au mataifa ya kale yalivyomchukulia mwanamke ndani ya jamii zao na mahusiano pamoja naye.

Historia inaonyesha namna hali ilivyokuwa mbaya, kwa Wayunani mwanamke alikuwa anauzwa na kununuliwa kama bidhaa, hakuwa na haki yeyote ndani ya jamii, katika jamii yao mwanaume ndiye

aliyekuwa na haki zote. Hakuwa na haki ya kurithi au kumiliki na kutumia mali.

Hali ilifikia kiwango cha mwanafalsafa wao maarufu anayeitwa Socrates kusema; "Kwa hakika kuwepo kwa mwanamke ndio sababu kuu na chanzo cha kuporomoka kwa maadili katika ulimwengu, kwa hakika mwanamke anafanana na mti wenye sumu, kwa nje yake unakuwa mzuri wa kupendeza, lakini kama ndege wakithubutu kuula tu, basi watakufa papo hapo!

Warumi wao walikuwa wanaitakidi kwamba mwanamke hana roho na wala kwao hakuwa na nafasi yoyote ndani ya jamii zaidi ya kifaa tu cha anasa kwa wanaume. Walikuwa wanafundisha kabisa kwamba, "mwanamke hana roho." Na kwa maana hiyo wakawa wanawaadhibu kwa kuwamwagia mafuta ya moto mwilini. Na wakati mwingine kuwafunga kwenye nguzo za miti juani kwa muda mrefu. Na wakati mwingine walikuwa wakiwafunga wanawake wasiokuwa na hatia kwenye mikia ya farasi na kuwaburuza mitaani mpaka wanakufa.

Na vivyo hivyo, kwa Wahindi, lakini wao walizidisha mabaya zaidi ya hayo, wao walikuwa wanamchoma moto mwanamke hai pale tu anapofiwa na mumewe! Wachina wao walikuwa wakimfananisha mwanamke

na maji yenye kuumiza yanayoosha au kuondoa furaha na mali! Enzi hizo mchina alikuwa na haki ya kumuuza mkewe, kama alivyokuwa na haki ya kumzika akiwa hai.

Mayahudi nao walikuwa na mambo yao, wao walikuwa wanamchukulia mwanamke kama kiumbe aliyelaaniwa, kwa sababu ya kumhadaa Adamu na

kumfanya ale tunda kutoka kwenye mti aliokatazwa.

Na humuona kuwa najisi pale anaingia katika siku zake, yaani walikuwa wanaamini kwamba anapopata hedhi alikuwa anainajisi nyumba na kila anachogusa. Kwao mwanamke alikuwa hana haki ya kumrithi baba yake kitu chochote, pale anapokuwa na kaka zake.

Ama Manaswara wanamuona mwanamke kuwa shetani! Mmoja katika wanazuoni wa Kinaswara amepata kusema; “Kwa hakika mwanamke hana mafungamano na jinsi ya binadamu.” Na mtakatifu Bonaventure amepata kusema; “Mnapomuona mwanamke nyinyi msidhani kuwa mmemuona binadamu au mnyama, kwa hakika huyo mnaemuona ni shetani na sauti mnayoisikia ni mlio wa nyoka.”

Na wanawake enzi hizo waliendelea kuishi kwa mujibu wa kanuni za nchi ya Uingereza, mpaka

katikati ya karne iliyopita, ambapo walikuwa hawachukuliwi kama raia, kama vile ambavyo hawakuwa na haki zozote, hata zile ambazo siku hizi wanaziita haki za kibinadamu. Mwanamke hakuwa na haki ya kumiliki kitu chochote hata mavazi yake mwenyewe ambayo anavaa! Kwa hakika Bunge la Uskochi (Scotland) la mwaka 1567M lilitunga sheria kwamba haifai kwa mwanamke kupewa uongozi wowote ule, kama ambavyo Bunge la Uingereza lilivyotunga sheria ya kumzuwia mwanamke kusoma Injili, wakati wa utawala wa Henry wa nane, kwa sababu waliamini kwamba mwanamke ni najisi.

Na katika mwaka 586M, Wafaransa waliweka kongamano la uchunguzi kuhusu mwanamke, hivi alikuwa mtu au sio mtu! Na wakapata majibu kwamba ni mtu lakini aliyeumbwa kwa ajili ya kumtumikia mwanamume.

Na mpaka kufikia mwaka 1805M sheria nchini Uingereza ilikuwa inaruhusu mwanaume kumuuza mkewe, na kulikuwa kumewekwa na kiwango hasa cha thamani yake kuwa pensa (pence) sita (yaani sawa na nusu shilingi).

Ama kwa Waarabu kabla ya Uislamu, mwanamke hakuwa na thamani yoyote, hakuwa na haki ya kurithi wala ya kumiliki mali ndani ya jamii! Ilifikia

hatua mtu akizaa mtoto wa kike, kwa sababu ya kuona haya ndani ya jamii mtu alikuwa anamzika mtoto wake wa kike akiwa hai.

Hii ndio ilikuwa hali katika ulimwengu huo kabla ya kuja kwa Uislamu.

Uislamu kimsingi, pamoja na mambo mengine ulikuja kuondoa dhulma zote dhidi ya mwanamke, Uislamu kupitia Kitabu chake Qur'ani umebainisha haki kama haki kwa wote, mwanaume na mwanamke kwa mujibu wa hali zao. Ndani ya Qur'ani Allah-Mtukufu Amesema; "Enyi watu, kwa hakika Sisi Tumekuumbeni nyinyi kutokana na mwanaume mmoja na mwanamke mmoja, na Tumekufanyeni nyinyi kuwa mataifa mbalimbali na makabila ili nyinyi mpate kujuana (katu Si kwa nyinyi kubaguana). Kwa hakika mtukufu wenu nyinyi mbele ya Allah-Mtukufu ni yule aliye mcha Mungu zaidi kati yenu. Kwa hakika Allah-Mtukufu daima ni Mjua-yote, Muelewa-yote." [Al-Hujurat, Q49:13].

Na katika Sura nyingine Allah-Mtukufu Amesema; "Na yeyote anayefanya yaliyo mema awe mwanaume au mwanamke huku yeye ni muumini, basi, hao wewe wataingia Peponi na katu wao hawatadhulumiwa chochote hata kama kikiwa na

ukubwa wa chembe ya kiuzi kwenye kokwa la tende." [An-Nisai, Q4:124].

Na Amesema tena Yeye Aliyetakasika na mapungufu yote; "Na Sisi Tumemuusia mtu wema kwa wazazi wake wawili, lakini kama wao wawili wakikulazimisha wewe ushirikishe pamoja Nami kile ambacho katu wewe huna elimu nacho, basi, katu wewe usiwatii wao wawili. Kwangu Mimi ndio marejeo yenu nyinyi na Mimi Nitakujulisheni nyinyi kuhusu yale ambayo nyinyi mlikuwa mnafanya." [Al-Ankabut, Q29:8].

Na Mtume - Rehema na amani ya Allah - iwe juu yake amesema; *"Mkamilifu wa imani miongoni mwa waumini ni yule aliye mzuri wao kitabia. Na watu bora kwenu nyinyi ni wale wabora wenu kwa wake zao kitabia."*

Na mtu mmoja alipata kumuuliza Mtume-Rehema na amani ya Allah iwe juu yake; 'Ni nani mwenye haki zaidi ya kutendewa wema (kati ya wazazi wangu wawili)?' Mtume - *Swallallaahu alayhi wasallama* akasema; *"Mama yako."* Yeye akasema tena; 'Kisha nani?' Mtume akasema: *"Mama yako."* Yeye akasema tena; 'Kisha nani?' Mtume akasema; *"Mama yako."* Yeye akasema tena; 'Kisha nani?' Mtume-

Swallallaahu alayhi wasallama akasema; *"Baba yako."*

Na huu ndio mtazamo na msimamo wa Uislam kwa ufupi juu ya mwanamke.

## Haki za Mwanamke kwa Jumla

Mwanamke katika Uislamu ana haki zake, kwa jumla ni kama zifuatazo;

1. **Haki ya kumiliki mali**; Katika Uislamu Mwanamke ana haki ya kumiliki chochote cha halali anachotaka au alicho na uwezo wa kukimiliki; Nyumba, mashamba, viwanda, bustani, dhahabu na fedha na aina ya mifugo, farasi, ngombe na kadhalika awe ni mke wa mtu, mwanamke mjane, mama, mtoto au dada.

2. **Haki yake ya kuolewa;** Mwanamke katika Uislamu ana haki ya kuchagua mume, kujivua kutoka kwenye ndoa, kudai talaka kwa sababu za kisheria, Na hizi ni haki zilizothibiti kwa mwanamke kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.

3. **Haki yake ya kupata elimu**; Katika Uislamu kutafuta elimu ni faradhi kwa mwanaume na mwanamke pia. Mtume - Rehma na amani ya Allah iwe juu yake amesema; *"Kutafuta elimu ni lazima kwa kila Muislamu."*

4. **Haki yake ya kutoa sadaka**; Mwanamke katika Uislamu ana haki ya kutoa sadaka kutoka kwenye mali anayemiliki, chochote atakacho, anaweza kujihudumia mwenyewe kutoka kwenye mali yake, na kumpa yeyote anayemtaka kama vile, mume, watoto, wazazi wake na kadhalika.

5. **Haki yake ya kuusia**; Mwanamke wa Kiislamu anaruhusiwa kuusia theluthi ya mali yake wakati wa uhai wake. Kwa sababu usia ni haki ya mtu binafsi, kama ilivyo kwa mwanaume ndivyo ilivyo kwa mwanamke. Kwa sharti wasia usizidi theluthi ya mali (⅓) husika. Katika jicho la sheria mwanamke na mwanamume ni sawa.

6. **Haki ya mavazi**; Katika Uislamu mwanamke ana haki ya kuvaa nguo na mapambo anayotaka kama

hariri na dhahabu, vitu ambavyo ni haramu kwa wanamume wa Kiislamu. Kwa sharti la kutochupa mpaka wa kisheria mbele ya wale ambao haruhusiwi kuonyesha mwili wake na mapambo yake.

7. **Haki yake ya kunywa na kula**; Katika Uislamu mwanamke anaruhusiwa kunywa na kula chochote anachopenda kwa kuzingatia sheria ya vya halali na haramu.

Allah Mtukufu Amesema: "Enyi wanadamu! Chukueni mapambo yenu kila wakati wa swala na kutufu na kuleni na kunyweni na katu nyinyi msifanye israfu, kwani kwa hakika (Allah-Mtukufu) katu Yeye Hawapendi wale waliyo wabadhirifu." [Al-A'raf, Q7:31].

Na maelekezo haya yanakusanya jinsia zote mbili (mwanaume na mwanamke).

8. **Haki ya Mirathi**; Katika Uislamu mwanamke ana haki ya kurithi na kurithiwa pia kwa mujibu wa sheria.

## Haki za Mke kwa Mumewe

Kwa hakika haki maalumu za mke ni zile haki kwa mumewe, ambazo kimsingi ni hizi zilizowekwa kwa mujibu wa sharia za ndoa, kama Allah-Mtukufu Anavyobainisha ndani ya Qur'ani; "Na wana wao (hao wake juu ya waume zao haki) mfano wa zile zilizo juu yao kwa wema. Na wanaume juu yao wana daraja. Na daima Allah-Mtukufu ni Mshinda yote, Mwenye Hekima (katika utendaji Wake)." [Suuratul Baqarah, Q2:228].

Ni wajibu kwa mume kumtekelezea mke wake haki zake kwa ukamilifu kwa kadiri ya uwezo wake, isipokuwa tu pale mke atakaposamehe baadhi ya haki zake ni lazima kwa mume;

1. Kumhudumia mke wake kwa jimai, chakula, vinywaji, mavazi na makazi.

2. Kulinda heshima ya mke wake, mwili wake, mali yake, na Dini yake.

3. Kumfundisha yaliyo lazima kuyajua katika mambo ya Dini. Kama atakuwa hawezi kulifanya hilo yeye mwenyewe, basi atampa idhini ya kujifunza kwa kuhudhuria darasa la wanawake kwenye nyumba za

Allah-Mtukufu, yaani Misikitini au mahali pengine palipoandaliwa kwa ajili hiyo.

Kuishi nae vizuri, kwa mujibu wa kauli ya Allah-Mtukufu; "Na muishi nao kwa wema." [An-Nisai, Q4:19]. Kuishi nao kwa wema ni pamoja na kutovunja haki zake, ikiwemo tendo la ndoa, na kutomuudhi kwa matusi, kumpuuza na kumdharau, kutomzuia yeye kuwatembelea ndugu na jamaa zake kama haogopi fitna kutoka kwa mkewe. Mume hatakiwi kumlazimisha mkewe kufanya kazi asizoweza. Kwa ujumla ni kufanyia wema kwa maneno na matendo kwa mujibu wa kauli ya Mtume - Rehema na amani ya Allah iwe juu yake; *"Mbora wenu nyinyi ni yule aliye m-bora kwenu kwa familia yake, na mimi ni m-bora wenu kwa familia yangu".*

## Hijabu

Pamoja na mambo mengine Uislamu umekusudia kuilinda jamii dhidi ya maadili potovu na kuijenga familia katika misingi inayokubalika, yaani ya Dini ya Allah-Mtukufu. Kwa kuweka uzio madhubuti, ambao ni adabu na tabia njema. Ili nafsi zibaki salama, Uislamu umeweka mipaka ili kuzuia visababishi vinavyoongoza kwenye mambo machafu ya zinaa,

ndio ukaamrisha kuinamisha macho kwa wanaume na wanawake.

Ndio Allah-Mtukufu Akafanya jambo la Hijabu kuwa sheria kwa mwanamke kwa ajili ya kumtukuza, na kumlinda kutokana na kudharaulika, na kumueka mbali na mambo ya mafisadi na watu wenye nafsi dhaifu katika wanaume, na hivyo kufunga mlango wa fitna kwa kumzuwiya mwanamke kudhihirisha yale yanayo fitinisha.

## Ndoa ya Wake Wengi.

Kwa hakika jambo la ndoa za wake wengi lilikuwepo miongoni mwa jamii katika historia ya binadamu. Na lilikuwepo pia kwenye sheria zilizotangulia kabla ya Uislamu na kwenye jamii za zamani pia, kama ilivyokuwa kwa Mayahudi, Manaswara, Wachina, Wahindi na wengineo. Na kuoa hakukuwa na idadi maalum, mwanaume alikuwa anaweza kuoa idadi ya wanawake anayotaka. Uislamu ukaja na kuondoa dhulma hii kwa mwanamke, na ukaweka idadi ya kuoa wake wengi kutozidi wake wanne.

Uislamu ulipohalalisha kuoa wake wengi uliweka sharti, nalo ni uadilifu kati ya wanawake na ukatoa tahadhari kubwa dhidi ya kuvunja sharti hilo na kuweka adhabu kali kwa mwenye kwenda kinyume.

Kilichozingatiwa na Uislamu katika kutoa ruhusa hiyo ni hali halisi na mazingira ambayo binadamu wanaishi kwa kuwa kuna dharura za kutosha zinazoweza kumfanya mwanaume kutaka kuwa na mke zaidi ya moja. Kwa mfano, mke wa kwanza anaweza akawa tasa, yaani asiyeweza kuzaa. Sasa katika hali hiyo mtu anaweza kuoa mke wa pili ili aweze kupata mtoto. Si lazima kumwacha huyo asiyezaa ili kuoa mwingine kwani kufanya hivyo ni aina fulani ya dhulma, kwa sababu hali hiyo Si ya kujitakia!

Dharura nyingine ni ajali, mke anaweza kupata na ugonjwa ambao kwa namna moja au nyingine akawa hawezi kumtimizia mumewe haki ya jimai! Katika hali kama hii pia mtu anaweza kuoa mke mwingine kwa sababu hiyo. Swali la kimantiki hapa ni je ni lipi jema kwa mke mwenye matatizo kama hayo, ni kuachwa na mume wake au ni mume kuoa mke mwengine?

Na kuna huu ukweli ambao uko wazi, kwa idadi wanawake ni wengi kuliko wanaume, kuoa wake wengi kwa mujibu wa sheria kutasaidia kupunguza idadi ya wanawake wazururaji mitaani bila ya waume na kwa hivyo kuwasaidia kujiepusha na zinaa!

Historia inaonyesha kwamba vita vya kwanza na vya pili vya dunia vilifanya wanawake zaidi ya milioni 25 kuwa wajane, baada ya waume zao kuuwawa vitani

katika nchi za Ulaya! Hivi ni lipi lililo bora, ni hawa wanawake kubaki bila kuolewa au ni kuolewa kama wake wa pili na hivyo kupata stara na hifadhi ya kijamii? Historia inathibitisha pia kufanyika kwa maandamano makubwa ya wanawake nchini Ujerumani baada ya vita ya pili ya Dunia mnamo mwaka 1945, ambapo wanawake walidai itungwe sheria (Kikatiba) ambayo ingeruhusu wanaume kuoa wanawake wengi kwa lengo la kuwalinda wanawake wa Kijerumani kujiingiza katika biashara ya ngono.

## Nini Uislam Unataka Kutoka Kwetu?

Uislamu haumtaki Muislamu kuipiga pande dunia moja kwa moja, wala hautaki watu wakae Misikitini tu wakifanya ibada, sivyo hivyo! Jambo la kwanza kabisa ambalo Uislamu unahimiza ni kutafuta elimu na la pili ni kufanya kazi ya kujipatia kipato cha halali kwa kuwa hiyo ndio njia pekee ya mtu kuweza kujikimu kimaisha yeye na familia yake!

Uislamu unataka Waislamu wawe watu walioendelea katika nyanja zote za maisha na *Alhamdulillahi* hilo lilifanyika kuanzia wakati Mtume Muhammad - *Swallallaahu alayhi wasallama* - aliposimamisha dola ya Kiislamu duniani mpaka mwisho wa Ukhalifa wa Sayyidina Ali bin Abi Twalib - Allah Amuie radhi. Fani mbalimbali za kielimu ziliendelezwa na kwa ujumla

Uislamu ulistawi kiasi cha kufikia hatua ya kukosekana watu wa kuwapa sadaka.

Kila Muislamu anatakiwa kujuwa pia haki za mwili wake kwake, kama kuupa chakula cha halali kizuri, kuupa mazoezi ya viungo na kuuliwaza kinafsi kwa jimai na starehe nyingine zilizo za halali. Na kuna haki ya kumtunza mke au mume na kuishi nae kwa wema na katu kutotoa siri zake kwa namna yoyote ile. Na kuna haki ya watoto kupata malezi mazuri ya kiroho na kimwili pia, bila ya kusahau haki za wazazi wake na ndugu na jamaa zake, bila ya kusahau haki na wajibu kwa jamii, kwa kufanya kila lenye manufaa na maslahi katika jamii. Na kubwa kabisa ni kutambua haki ya Allah-Mtukufu ya kumpwekesha na kumtii!

Uislamu unatubainishia sisi kwamba Allah-Mtukufu Ndiye Mmiliki wa mbingu na ardhi na vyote vilivyo ndani yake, na Yeye Hufanya Anavyotaka katikao, Yeye Huhuisha na Kufisha, Huacha watu kuuguwa na Huwaponya. Na Allah-Mtukufu Hutoa mali nyingi kwa yeyote Amtakaye na Hubana pia kwa yeyote Amtakaye, Huwajaribu watu kwa Kuwafanya masikini na wengine matajiri! Yeye Hurutubisha baadhi ya ardhi na nyingine Huifanya kuwa kame na nyingine jangwa, milima na mabonde.

Yeye Huwapa baadhi ya watu watoto wa kiume na wa kike, wengine Huwapa wa kiume tu na wengine Huwapa wa kike tu na wengine Hawapi kabisa, na yote hayo Yeye Huyafanya kwa hekima Yake iliyo nje ya upeo wa akili ya binadamu! Allah-Mtukufu Huwaandikia watu siku ya kufa kwao wakiwa bado matumboni mwa mama zao, kabla hawajazaliwa. Wengine Huwafisha kabla ya kuzaliwa na wakazaliwa wakiwa tayari wamekwishakufa, wengine hufishwa wakiwa wadogo, wengine katika utu uzima wao na wengine wakiwa vikongwe kabisa! Yeye Hunyesha barafu katika baadhi ya maeneo na Kusababisha baridi kali ya kufa mtu na maeneo mingine Yeye Huyafanya kuwa na joto la kutisha na kote huko watu wanaishi kama kawaida kufuatana na mazingira yao. Yeye Husababisha tetemeko la ardhi na Kubomoa majumba mengi na watu wengi pia kufa kwa wakati mmoja! Wakati mwingine Yeye Huachia meli kuzama baharini na watu wengi kufa maji na hivyo kuwa chakula cha samaki! Na yote hayo ni mambo ambayo binadamu hana uwezo wa kuyazuia. Kwa hivyo Yeye Kuwafanya watu wenye akili kubaini kwamba kwa hakika Allah-Mtukufu Ndiye Mmiliki hasa wa kila kitu na Ndiye Anayeendesha kila kitu barabara kama Alivyokwisha kadiria! Lakini je, huko kukiri tu ukweli huu kunatosha kupata mtu sifa ya kuwa Muislam?

Jibu ni hapana! Ili kuwa Muislamu mzuri ni lazima mtu, baada ya kukiri kwamba hapana Mola Anayepasa kuabudiwa kwa haki ila Allah-Mtukufu tu Peke Yake na kwamba Mtume Muhammad - *Swallallaahu alayhi wasallama* ni mja na Mtume Wake, kutekeleza nguzo zote tano za Uislamu kwa vitendo kwa kadiri ya uwezo wake, bila ya kushirikisha chochote kingine katika ibada Yake. Na huo ndio Uislamu.

Ni lazima kwa Muislamu kukiri pia kwamba manufaa na madhara yote hayo hupangwa na Allah-Mtukufu, kuhalalisha na kuharamisha ni haki ya Allah-Mtukufu tu Peke Yake, ni lazima mapenzi kamili na hofu kamili na utii mkamilifu vyote vielekezwe kwa Allah-Mtukufu tu. Kwa vyovyote vile moyo uliojaa dhikri ya Allah-Mtukufu na kutambua kwa hakika maana ya neno *Allahu Akbar*! Mungu Mkubwa, bila shaka utakiona kila kitu kuwa kidogo mbele ya Allah-Mtukufu.

Na ifahamike kwamba kuna katika matendo ya binadamu yenye kuashiria kutukuza kulikokamilika, kama vile kuomba dua na kuswali, kurukuu na kusujudu, kuweka nadhiri na kuchinja, kumtakasa Allah-Mtukufu na kumpwekesha na kila ushirikina. Kwa hakika Muislam hafanyi yote hayo isipokuwa kwa ajili kutafuta Radhi ya Allah-Mtukufu, basi haswali kwa ajili ya yeyote mwingine, wala hasujudu

na kurukuu isipokuwa kwa ajili Yake Yeye tu, Aliyetakasika na mapungufu yote! Wala yeye hamuombi mwingine yeyote asiyekuwa Allah-Mtukufu! Wala hatubu kwa dhambi aliyofanya ila Kwake Yeye tu Peke Yake. Yote hayo ni katika ishara za kutukuza kikamilifu, na jambo hili ndio msingi na siri ya ibada.

## Uislamu Unafuta Madhambi ya Kabla Yake.

Na katika Fadhila za Allah-Mtukufu na Rehema Zake kwa waislamu ni pale Alipoufanya Uislamu kuwa wenye kufuta yale ya kabla yake, katika madhambi kutokana na maasi mbalimbali. Basi, ndio ikawa kafiri anaposilimu Allah-Mtukufu Humsamehe makosa yake yote aliyotenda wakati akiwa kafiri na kuwa safi asiye na dhambi yoyote.

Na mtu aliyeneemeshwa na Allah-Mtukufu kwa kuwa Muislam, hata kama katika ukafiri wake alipata kuchuma mali kwa njia za haramu, mali hiyo inakuwa halali kwake. Kwani ndani ya Qur'ani Allah-Mtukufu Amesema; "Sema (ewe Mtume - *Swallallaahu alayhi wasallama*) kwa wale ambao wamekufuru kwamba yatasamehewa kwao yale yaliyotangulia (katika dhambi)…" [Al-Anfal, Q8:38]. Maana yake kwa Huruma Yake Allah-Mtukufu Atawatakasi na Kuwafanya kutokuwa na dhambi yoyote.

Isipokuwa mali aliyoipata kwa kudhulumu watu hiyo atapaswa kuirejesha kwa wenyewe! Ama mali aliyochuma kwa ridhaa za watu wenyewe, hata kama ikiwa ni ya haramu, kama mali ya riba au biashara ya mihadarati au biashara nyingine ambayo ni haramu kisheria, basi hiyo inakuwa halali kwake anaposilimu na ataendelea kuimiliki.

Ifahamike kwamba mlango wa toba katika Uislamu uko wazi, hata kama mtu atakuwa na madhambi sawa na wingi wa mchanga wa fukwe za bahari. Na mahitaji ya binadamu katika toba ni endelevu, kwa kuwa kila binadamu hufanya makosa, na mtu mwema katika wanaofanya makosa ni yule anayetubu baada ya kubaini kosa lake. Kama Mtume - *Swallallaahu alayhi wasallama* alivyosema; *"Kwa kuwa binadamu hana kinga inayomzuia kutenda dhambi, hakika Allah-Mtukufu Amemfungulia mlango wa toba na Amemuamrisha mtu kufanya hivyo pale anapokuwa ameteleza na kufanya kosa!"* Ndani ya Qur'ani Allah-Mtukufu Amesema; "Sema enyi waja Wangu wale ambao wamedhulumu nafsi zao katu nyinyi msikate tamaa na Huruma ya Allah-Mtukufu, kwa hakika Allah-Mtukufu Husamehe dhambi zote, hakika Yeye ni Mwingi wa Kusamehe, Mwingi wa Huruma." [Az-Zumar, Q39:53].

# Ni Vipi Mtu Huingia Kwenye Uislam?

Baada ya mtu kujuwa utukufu wa Dini ya Kiislamu na kujuwa kwamba hiyo ndio njia pekee ya kuokoka mbele ya Allah-Mtukufu na kwamba kuwa Muislamu ni jambo la asili na la lazima kwa kila mtu na kwamba hakuna njia ya kuingia Peponi na kuepushwa na Moto wa Jahanamu Siku ya Kiyama isipokuwa kwa kuwa Muislamu na ni jambo rahisi! Kwa asiyekuwa Muislamu anapotaka kuwa Muislamu ni lazima yeye aamini; Hapana Mola Apasaye kuabudiwa kwa haki ila Allah-Mtukufu, na kuwa Muhammad ni Mtume wa Allah, moyoni mwake na atamke kwa ulimi wake; Ash-hadu an laa ilaaha illa Llah wa ash-hadu anna Muhammadan rasuulu Llah, kisha aanze kujifunza ibada na sheria za Kiislamu kuhusu mambo mbalimbali na azitekeleze! Mfano ni kama ule wajibu wa kuswali mara tano kwa siku na kadhalika. Na vitabu vya kujifunza mambo hayo vimejaa maduka mbalimbali na vituo vingine vya Kiislam.

## VYANZO:


1. Dini ya Kiislamu
2. Njia kuelekea kwenye Uislamu
3. Silabasi ya elimu ya Familia na Jamii
4. Kuutambulisha Uislamu
5. Kongamano la wazi, la Mwenye Fadhila Sheikh Muhammad Bin Swalehe Al Uthaimini.

# YALIYOMO:

UTANGULIZI........................................................ 3

KWA NINI TUMEUMBWA?........................................ 6

UISLAM NI NINI?................................................... 7

KUUMBWA KWA NABII ADAMU ................................ 8

Mtume Muhammad - Rehema na Amani ya Allah-
Mtukufu iwe juu yake:........................................... 13

Misingi ya Dini ya Kiislam....................................... 33

NGUZO ZA UISLAMU ............................................. 42

Maana ya Nguzo za Uislamu .................................. 43

Baadhi ya Sifa za Dini ya Kiislamu. ......................... 47

Mambo Mazuri Yanayo Himizwa na Uislamu ................. 58

Matendo tunayoamrishwa kufanya...................... 58

Mambo tunayokatazwa kufanya.......................... 60

SIKU YA MWISHO ................................................. 64

Ishara za Kukaribia kwa Kiyama ............................. 73

Ukali wa Adhabu ya Moto ..................................... 77

Haki za Mwanamke katika Uislamu ......................... 82

Haki za Mke kwa Mumewe..................................... 91

Hijabu........................................................... 92

Ndoa ya Wake Wengi............................................ 93

Ni Vipi Mtu Huingia Kwenye Uislam?......................101

VYANZO:...........................................................102